

**MADA: METHALI KAMA FALSAFA YA MAISHA: UNAKIKI
LINGANISHI WA METHALI ZA KIKOREA NA ZA KISWAHILI**

Na

YANG CHUL JOON

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya
M.A. katika Chuo Kikuu cha Nairobi**

1992

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY




0101841 5

UNIVERSITY OF NAIROBI
LIBRARY


UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote




**Yang Chul Joon
(Mtahiniwa)**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii ya chuo kikuu



Prof. Mohamed Hassan Abdulaziz



Bw. Mwenda Mbatiah

TABARUKU

Tasnifu hii yatabarukiwa wazazi wangu, Bw. Yang Hee Sun na Bi.
Kim Byung Ah ambao wamejitolea kunielimisha na ambao
wamedhihirisha mafunzo yale ya Kichina:

"Kumpatia mwanao *sutra* moja ni bora kuliko kumrithisha kasha moja
linalojaa dhahabu tupu"

-Kitabu cha *Han*-

YALIYOMO**Ukurasa****UNGAMO****TABARUKU**

YALIYOMO.....	i
SHUKRANI.....	iii
MUHTASARI WA TASNIFU.....	vii

SURA YA KWANZA

1.1. Somo la utafiti.....	1
1.2. Madhumuni ya tasnifu.....	2
1.3. Sababu ya kulichagua somo hili.....	5
1.4. Upeo wa tasnifu.....	7
1.5. Msingi wa kinadharia.....	9
1.6. Yaliyoandikwa kuhusu somo hili.....	14
1.7. Njia za utafiti.....	18
Tanbihi.....	20

SURA YA PILI

2.0. Utangulizi.....	23
2.1. Ibada, miiko na ushirikina katika taswira za viumbe.....	26
2.2. Tamathali za usemi katika methali.....	36
2.3. Taswira za wanyama katika methali.....	43
Tanbihi.....	52

SURA YA TATU

3.0. Utangulizi.....	66
3.1. Upangaji wa methali.....	67
3.2. Uainishaji wa methali kimaudhui.....	70
3.3. Maana na matumizi ya methali kwa mbinu ya ulinganishi.....	83
Tanbihi.....	129

SURA YA NNE

4.1. Muhtasari wa kiini cha tasnifu	130
4.2. Ubia wa hisia za kibinadamu katika methali	132
4.3. Mapendekezo	134
Tanbihi.....	139
MAREJEO	141

SHUKRANI

Nawashukuru ghaya wazazi wangu, Bwana Yang Hee Sun na Bibi Kim Byung Ah ambao wameithamini elimu kama hazina ya maisha idumuyo milele na kutuelimisha kwa upendo na moyo safi kabisa wa kujitolea. Upendo wa wazazi wangu usiokuwa na kifani unaweza kulinganishwa na bahari isiyo na kikomo. Upendo wao vilevile umekuwa nguzo imara katika kila nifanyalo na hautasahaulika abadani, daima dawamu.

Shukrani za dhati nawatolea wasimamizi wangu, Profesa Mohamed Hassan Abdulaziz na Mwalimu Mwenda Mbatiah kwa usimamizi wao aula toka awali hadi aheri. Usimamizi wao wenye kutimirya na ustahamiliuu ulinitilia ari na ghera tangu mwanzo hadi mwisho na kutokomeza mitafaruku yoyote ya kiroho na ya kinafsi katika jitihada zangu za kuhitimisha kazi hii. Mashauri yenye kupendeza na kufaa yalikuwa kama jiwe la msingi na mchango muhimu kwa kazi hii.

Profesa Mohamed Bakari, Profesa Jay Kitsao, Mwalimu Kithaka wa Mberia, Mwalimu Gichobi Mungania, Mwalimu John Habwe, Mwalimu Kineene wa Mûtiso na Mwalimu Ken Osinde nawashukuru upeo wa shukrani kwa kunipanulia ujuzi wa lugha na fasihi ya Kiswahili na kwa kunipatia mtazamo mpya wa kiulimwengu. Wasomi hawa wanaofungua ukurasa mpya wa utukuzaji na usambazaji wa lugha tukufu ya Kiswahili ndio watangulizi ambao wadhihirisha funzo la methali hii;

"Nia zikiwa moja, kilicho mbali huja".

Dilevile siwezi kumsahau Profesa Lucia Omondi ambaye ndiye nahodha wa Idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mawaidha yake na usaidizi wa kila namna.

Aidha namshukuru sana Mwalimu K.K. Kahigi kwa takirima yake. Kila mara nilipozuru Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alinisaidia kwa mashauri mema na udugu.

Ningependa pia kuwashukuru Profesa Kim Youn Jin na Profesa Kwon Myong Shik kwa kuniongoza kwenye ulimwengu wa lugha na fasihi ya Kiswahili na kwa kuniwekea jiwe imara la msingi kwa jengo langu la kiusomi. Lau si mwongozo wao nisingeweza kupata fursa ya kung'arisha ufasaha wa lugha ya Kiswahili.

Hali kadhalika upeo wa shukrani nampa Profesa Miyamoto Masaaki kwa kunitia moyo kama ndugu wa kiusomi na kwa kunihimiza kama mufti apevukaye. Mahimizo yake yamechangia sana maendeleo ya masomo yangu na kuniwezesha kupanua upeo wangu wa kiusomi.

Ni wajibu wangu pia kuwashukuru Bwana Cho Nam Doo, Bwana Son Young Mog, Bwana Yook Byung Kuk na Bibi Cho Hye Ok kwa ukarimu na usaidizi wa kila namna.

Waidha wakufunzi wenzangu ambao wamenipatia mashauri, maoni na mahimizo bora yafaayo katika masomo yangu walidhihirisha funzo la ile methali ya Kiswahili; "Kutoa ni moyo, usiambe ni utajiri." Udugu na urafiki wetu utajengua ukuta wowote kati yetu na kuleta mshikamano wa kiusomi. Kyallo wadi Wamitila, Amiri Swaleh, Margaret Wangari Njuguna, Teresa Wambui Baru na Florence Mugure Wamakima wastahili kupewa upeo wa shukrani.

Vilevile ningependa kusheheneza shukrani zangu za moyo kwa Bw. na Bi. Mutundu ambao wamejitolea kupiga taipu kazi hii iwe maridadi na maridhawa. Usafi wa moyo wake nitaukumbuka moyoni mwangu daima dawamu.

Isitoshe, sitasahau kuwashukuru masahibu wangu kwa umbuya wao na hisani yao ya kila aina. Masahibu hao ni Mirande Jaeckx, Ann Lynae Bruce, mkufunzi wa Chuo kikuu cha Shippensburg Marekani, Kristine Han, Fairouz Jacobs, Masumura Keiko, Nakahashi Kazuaki, Bwana na Bibi Yamaguchi Akihiko, Bwana na Bibi Fujinaka Katsunori wa Shirika la Kimataifa la Japan (Japan International Cooperation Agency), Hagen Neumueller, Akio Nishiura, Rika Miyachi, Monique Winzong, Renee Ankarfjard, Azam Dabirzadeh, Yamamoto Ryoji, Dagmar Hornnich, Engi Emese, Profesa Ram B. Ramchandani wa Chuo Kikuu cha Bombay nchini India, Simonetta Rigato, Arja Paananen, Hanne Nysom, Tina Ljungstrom, Nina K. Sollid, Marion Niessen, Dawn Jennings, Hojdeh Ghorbani, Hu Shanshan, Elizabeth LeDieux, Mungai wa Mutonya, Christina Lee, Chris Koch, Tsunoda Mitsuaki, Dirk Nolte, Flemming

Laugesen, John Saliba, Vincent Ogutu, Bellanger Patrick, Maria Nieves Fdez, Hanae Ezashi, M. K. Yahaya, Lee Dong Chul, Ko You Na, Kim Yong Jae, Kang kyung Sup, Park Young Sun, Chung Ran Kyung, Chun Yoo Sun, Lee Moon Young, Ham Eun Mi, Patricia Thoronjo, Irene Ngina, Emily Divers na Shin Chang Hee.

Hali kadhalika ningependa kuzitoa shukrani zangu za dhati kwa kakangu Yang Duk Joon na dada zangu wawili Yang Jeong Sook na Yang Ae Yi kwa upendo wao na udugu.

Pasingekuwa na usaidizi wa wengi usiojua kuchoka kazi hii ingekwama njiani na isingepata nuru ya ulimwengu huu murua.

MUHTASARI WA TASNIFU

Tasnifu hii ni uhakiki linganishi wa methali za Kikorea na za Kiswahili. Methali kama fani moja ya fasihi simulizi hujumuisha fikira na mawazo mbalimbali ya umma na hivyo basi methali ni kiini cha hekima zinazochujwa na kusimuliwa katika maisha halisi ya binadamu. Tasnifu hii imeshughulikia maudhui mbalimbali yanayotiririka katika methali.

Tasnifu hii imekusudiwa kuangalia jinsi watu wanavyofikiria kuhusu maswala mengi yanayojitokeza katika maisha ya binadamu kwa mbinu ya kuzilinganisha methali za jamii mbili. Zaidi ya hayo tumeazimu kuthibitisha ubia wa hisia za kibinadamu kupitia kwa methali.

Methali za Kikorea na za Kiswahili zinazokusanywa na kulinganishwa katika tasnifu hii zitawapatia wasomaji fursa ya kufahamu utamaduni wa Wakorea na Waswahili. Kama kazi ya uasisi ambayo ingepatikana na udhaifu hapa na pale, tasnifu hii ingeshambuliwa kiusomi na kuhakikiwa kwa undani na upana ndipo tutafanikiwa kupanua utafiti wa fasihi simulizi methali ikiwemo na kuinua kiwango cha uhakiki.

Tasnifu hii imejengeka na sura nne. Sura ya kwanza imeandikwa kuhusu baadhi ya mambo yaliyo muhimu kama jiwe la msingi katika kutimiza matilaba ya tasnifu hii. Hayo ni somo la

utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu za kulichagua somo hili, upeo wa tasnifu, msingi wa kinadharia, yale yaliyoandikwa kuhusu somo hili na njia za utafiti.

Katika sura ya pili tunashughulikia ibada, miiko na ushirikina katika taswira za wanyama mbalimbali. Tunatoa mifano kadha wa kadha ili kueleza chimbuko la imani hizi. Kwa kuwa imani hizi zina umuhimu katika kufahamu jinsi binadamu na mazingira yanayowazingira yanavyoingiliana na kuathiriana, tunazijadili imani hizo kwa kutoa methali kama mifano au ithibati za kuonyesha maswala haya.

Pia tunaeleza tamathali za usemi katika methali. Ingawa tamathali za usemi katika methali ni upande wa fani na sura, kuzifahamu tamathali za usemi kunatusaidia kuchambua maudhui na ujumbe katika methali. Aidha tunashughulikia taswira za wanyama wanaojitokeza mara kwa mara katika methali za Kikorea na za Kiswahili. Taswira hizo ni muhimu sana katika kuzifahamu methali na mara nyingine ni vigumu sana kuzifahamu methali bila kuzielewa taswira hizo.

Sura ya tatu katika tasnifu hii inahusu upangaji wa methali, uainishaji wa methali kimaudhui na maana na matumizi ya methali za jamii ya Wakorea na ya Waswahili. Tunafafanua mbinu ya kuzipanga methali katika tasnifu hii kusudi wasomaji waweze kuzilinganisha kwa urahisi. Fauka ya hayo mbinu mbili

zilizotumiwa kuziainisha methali kimaudhui na C.L. Sibusiso Nyembezi (1963) na Chung, Chong Hwa (1991) zinaelezwa kwa kusudio la kuonyesha jinsi mbinu mbalimbali zinavyohitilafiana katika uainishaji huo wa kimaudhui. Kisha tunafafanua maana na matumizi ya methali za Kikorea na za Kiswahili kwa mbinu ya ulinganishi. Hii ndiyo sehemu ya uti wa mgongo katika tasnifu hii.

Sura ya nne ni ya mwisho katika tasnifu hii. Tunapitia kiini cha tasnifu kwa muhtasari. Tumetaja baadhi ya mambo muhimu yanayoibuka katika kazi ya uchunguzi wa fasihi simulizi hasa methali kwa ufupi. Kwa kuzitoa methali za jamii mbalimbali zenye maana moja, tunaeleza ubia wa hisia za kibinadamu katika methali. Hatimaye tunatoa mapendekezo yetu ambayo ni mwito wetu.

SURA YA KWANZA

1.1. Somo la utafiti

Kulingana na fasihi andishi kama vile riwaya, insha, tamthilia na mashairi, utafiti mpana kuhusu fasihi simulizi haujafanywa kwa undani, ilhali fasihi simulizi inastahili kutiliwa umuhimu na maanani kwa kuwa fasihi simulizi huwa ni kazi ya umma ambayo huwakilisha fikira na mawazo ya wanajamii fulani.

Hatuwezi kukanusha ule ukweli uliopo kwamba watafiti wa fasihi wamejipusha na fasihi simulizi wakiihusisha na ushenzi ama mambo ya kitoto ambayo yangeturudisha nyuma kufikia kwenye kiza totoro. Chambilecho S. A. Khamis (1983):

Hata katika wakati huu, bado tunaambiwa: 'ustaarabu', hasa yale yanayoambatana na ubepari, ndio upasao kusifiwa kwamba ulichukua sehemu kubwa ya kufutilia mbali alama au mabaki ya ile fasihi ya 'kishenzi'; yaani fasihi simulizi. (1)

Kusema kweli hatujahisi kujitupilia mbali kwa kufutilia mbali na kuacha kando urithi wa kijadi ikiwemo fasihi simulizi, hasa methali ambazo tutazishughulikia. Maendeleo kwa dhana ya mabepari yamedhoofisha maisha ya kijumuia na kuharakisha jamii ya kibinafsi ambapo fasihi simulizi hupuuzwa na kudidimia. Zaidi ya hayo wakoloni walishika kani kutokomezwa utamaduni wa kitaifa na kuimarisha mfumo wa kikoloni kwa kuwafanya watawaliwa wa koloni wajikanushe na kujidunisha wenyewe. Hatuwezi kukanusha kwamba utamaduni wa Ulimwengu wa Tatu umenajisiwa na utamaduni wa kikoloni na kibeberu

kwa kiasi ambacho watu wa nchi changa za Ulimwengu wa Tatu wanaudharau na kuuhafifisha utamaduni wao.

Wataalamu wengi wenye mwamko wa kitaifa umeanza kufanya utafiti kuhusu utamaduni wao ikiwemo fasihi simulizi. Hao wanajaribu kuwahimiza vijana wa kizazi hiki na kijacho wajionee fahari utamaduni wao wa kijadi na kujitukuza. Wanakutana na busara na hekima ya mababu zetu kwa vile methali ilikuwa chombo muhimu cha kuhifadhi roho ya kitaifa. Methali huwa inatuonyesha tajiriba na tabasuri ya watu. Dilevile methali huhuisha mazungumzo ya kawaida na methali kimsingi ni fasihi ya maisha.

Umuhimu wa methali ni kwamba methali huchukua nafasi katika jamii zikichujwa na maoni na hisia za ndani za wanajamii. Ubunifu wa mtu mmoja unaanza kuwa na uhai na kukubaliwa miongoni mwa wanajamii na unakuwa fasihi ya umma.

Kwa sababu hii chombo kimojawapo cha kuzilinganisha jamii mbili ni methali. Katika kazi yetu tutajaribu kuzilinganisha methali za Kikorea na za Kiswahili kwa minajili ya kuangalia tofauti zilizopo na makaribiano yaliyopo ambayo ni muhimu kuziba pengo la kiutamaduni.

1.2. Madhumuni ya tasnifu

Umbali wa kijiografia baina ya eneo la Mashariki ya Mbali lenye nchi kama Korea, Japan na China na eneo la Afrika Mashariki umekuwa sababu ya kutoingiliana na ya kutowasiliana kiutamaduni, kiuchumi na

kisiasa. Ingawa Wachina walikuwa wamewasiliana na watu wa Afrika Mashariki kwa madhumuni ya biashara za pembe za ndovu na kifaru, inaaminika kwamba hakukuwa na mawasiliano halisi kati ya maeneo hayo mawili kabla ya karne ya ishirini.

Kufuatana na taarifa inayopatikana kwenye kitabu cha Historia ya Afrika Mashariki kilichohaririwa na Roland, Oliver na Gervase, Mathew (1963);

Kufikia karne ya kumi wanajiografia wa China walimakinika kujua njia *Po Pa Li* iliyokuwa katika Bahari ya Magharibi na kusikia kuhusu mila za wenyeji weusi walio wakali wa *Mo Lin*. Yaaminika kwamba *Po Pa Li* ilikuwa sehemu fulani ya pwani ya Somali na *Mo Lin* ilikuwa sehemu ya Malindi. Inaelekea kwamba hadithi hizi zilikuwa uvumi uliokusanywa katika Bara Hindi au Indonesia. Zaidi ya hayo, kulikuwa na biashara ya watumwa. Mnamo mwaka wa 614 Baada ya Kuzaliwa kwa Yesu Kristo, wajumbe kutoka kisiwa cha Java waliwaletea wanawake wawili wa *Seng-Chi* kama zawadi iliyotolewa kwa mfalme; wakati wa karne ya nane wanawake wafupi wawili na wanawake wawili wa *Seng-Chi* walizawadiwa kwa mfalme na mtawala wa *Sri Iijaya*. Mnamo mwaka wa 1119 matajiri wengi wa Jimbo la *Canton* waliwamiliki watumwa weusi. Mabori, pembe za vifaru, magamba ya makobe na ambari ni baadhi ya malighafi ambayo yalikuwisha julikana katika ufalme wa China kama bidhaa za nchi ya Zanj ya Weusi (2)

Historia hii ni maandishi yenye uchungu katika historia ya mawasiliano kati ya watu wa Mashariki ya Mbali na wale wa Afrika Mashariki. Mawasiliano ya namna hii yamebakisha mawaa yasiyofutika kwenye historia.

Wakorea na Wajapani hawakuwa na mawasiliano maalum na watu wa Afrika Mashariki kufikia katikati ya karne ya ishirini. Ni dhahiri kwamba kutowasiliana huku kumejenga ukuta mrefu tena mgumu wa kutofahamiana ambako ndiko chanzo cha kusababisha taasusi ya kitaifa miongoni mwa wanadamu.

Utafiti wa methali unaweza kuwa njia moja ya kufahamiana kwa vile methali ni chombo muhimu cha kuwakilisha fikira na mawazo ya watu. Kama fani moja ya fasihi simulizi, methali ni fasihi ya umma ambao ni wajenzi wa historia wanaoendeleza magurudumu mawili ya maendeleo. Chambacho Kim, Dae Jung (1984):

Umma ni halaiki ya watu ambao wako katika msingi wa matabaka ya kijamii, lakini wananyongwa, kutawaliwa na kudhulumiwa vibaya, ilhali wanazalisha mali. (3) (tafsiri yetu)

Tuna imani thabiti ya kwamba uhakiki wetu wa methali za Kikorea na za Kiswahili utaweka msingi imara kwa lengo la kufahamiana kwa tamaduni za Wakorea na wale wa Afrika Mashariki. Haya ndiyo madhumuni makuu ya somo letu.

Katika somo kama hili, linalopaswa kuzingatiwa ni kwamba lazima tuwe na msimamo na mtazamo unaofaa toka mwanzo mpaka mwisho. Ni dhahiri kwamba wataalamu wengi wamenadharisha ubora na uduni wa wanadamu katika utafiti na uchunguzi wa mambo ya Ulimwengu wa Tatu.

Uhakiki wetu utaongeza mchango mdogo, lakini twatumai muhimu katika harakati za kuipa sura ya kimataifa lugha ya Kiswahili. Hatuwezi kutarajia usambazaji na utukuzaji wa lugha ya Kiswahili bila kuoanisha nia yetu na harakati zetu za kuikamilisha nia hiyo.

1.3. Sababu za kulichagua somo hili.

Swali ambali lingeweza kuulizwa ni kwa nini tumechagua somo hili la uhakiki linganishi wa methali, ilhali kuna tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kama vile vitendawili, ngoma, ngano, hadithi, majigambo, nyimbo na hurafa ambazo vilevile hazijafanywa utafiti wa kutosha, sababu kadha wa kadha zinazoweza kutolewa kulijibu swali hili ni kama zifuatazo;

Kwanza ngoma, nyimbo na vitendawili huwa zinazotolewa kuwaburudisha watu na kuwasaidia wachemshe bongo. Tanzu hizi za fasihi simulizi hutumiwa katika hali na miktadha maalumu. Lakini methali, kingume cha matumizi ya tanzu nyingine za fasihi simulizi, hudondoleka mara nyingi hasa wakati tunapokusudia kutilia mkazo mazungumzo yetu ya kila siku. Twaweza kufupisha mazungumzo marefu ya kuwachochoa wasikiao kwa kuzitoa methali wakati panapofaa. Kwa vile methali hutolewa mara nyingi katika maisha yetu ya kila siku, ni rahisi kukusanya data za kutosha kuzichambua.

Pili, methali hutuonyesha kiwango cha juu katika matumizi ya sitiari ambayo hulinganisha vitu na viumbe kana kwamba vitu na viumbe hao ni sawa. Matumizi haya yanatuonyesha fikira na mawazo

ya wanajamii kuhusu swala fulani moja kwa moja kuliko tamathali zingine za usemi. Baadhi ya mifano ni kama ifuatayo;

- . Urembo ni urimbo.
- . Mkataa kwao ni mchawi.
- . Ujana ni moshi.
- . Dunia ni mti mkavu.
- . Hasira ni hasara.
- . Rhadi ni deni.
- . Subira ni ufunguo wa heri.
- . Majuto ni mjukuu.
- . Muungwana ni kitendo.
- . Kukasirika ni kughururika. na kadhalika.

Kama tuliivyotaja hapo juu, matumizi ya sitiari katika methali hutuwezesha tuwe na ujuzi kuhusu mitazamo na mielekeo ya watu wenye tamaduni zitofautianazo kabisa kuhusu matukio mbalimbali ya maisha. Kwa hakika mitazamo na mielekeo hiyo huhusiana na kuchangamana na falsafa ya jamii husika.

Tatu, methali ni fasihi ya umma kimsingi ambayo inawakilisha falsafa ya maisha. Utafiti wa methali ndilo sharti la kimsingi ambalo ni muhimu sana kutambua tofauti zilizopo na makaribiano yaliyopo. Tusipofahamu zile tofauti za kiutamaduni za wengineo wasio wanajamii wenzetu, hatutaweza kuliziba pengo la kiutamaduni ambalo huzuia ushirikiano na mafahamiano kati ya wanadamu wa mataifa mbalimbali ya ulimwengu huu.

Nne, methali ni kiini cha uteuzi wa maneno. Twaweza kutathimini na kutambua umahiri wa matumizi ya maneno. Tukiiangalia methali moja ya kiswahili;

. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

Methali hii inayosisitiza thamani ya ndugu na uhusiano mzito wa ndugu inatuonyesha kiwango cha juu katika uteuzi wa maneno.

1.4. Upeo wa tasnifu

Katika tasnifu hii methali zinazotumiwa kuhakikiwa ni zile methali za kikorea ambazo zinakaririwa katika korea kusini. Mara Wakorea walipojinyakulia uhuru kutoka kwa minyororo ya Wakoloni wa Japan Wakorea walilazimishwa kugawanyika. Sasa kuna Jamhuri ya Korea (Korea Kusini) na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Korea (Korea Kaskazini) katika Rasi ya Korea. Jamhuri ya Korea ni nchi ya kibepari na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Korea ni nchi ya kisoshalisti. Tofauti za mfumo wa kisiasa zimesababisha tofauti za mambo mbalimbali katika maisha ya Wakorea. Aghlabu tanzu mbalimbali za utamaduni huathiriwa na kuamuliwa na mfumo wa kisiasa na kiuchumi. Methali zilizotumiwa kabla ya Wakorea kujinyakulia uhuru zilikuwa sawa pasi na tofauti dhahiri, lakini methali zilizoundwa tangu uhuru zinatofautiana kwa kiasi kikubwa katika matumizi na maana. Hatutazihakiki methali za Kikorea zinazotumiwa

katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya watu wa korea kwa sababu haiwezekani kuzikusanya methali hizo. Kutoweza kuzihakiki methali za Kikorea zinazotumiwa katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Watu wa Korea kunatuhuzunisha na kutosikitisha mno, twatumaini methali hizo zitahakikiwa kabla ya siku si nyingi.

Kwa kawaida twaona ya kwamba maelezo ya matumizi na maudhui ya methali huhitilafiana kufuatana na maoni na mitazamo ya azichambuaye ama mhakiki. Hii inatufahamisha methali huwa na maana zaidi ya moja ambazo zingefahamika kwa namna mbalimbali kulingana na muktadha maalum. Ugumu wa kuziainisha methali kimaudhui huibuka kwa sababu hii. Digezo mbalimbali vitakavyotumiwa kuziainisha methali kimaudhui katika kazi yetu vitakuwa na ubinafsi wetu.

Jambo lingine lipaswalo kutajwa hapa ni kwamba mapigo ya kimuziki katika methali yangepotea na kudidimia katika kuzitafsiri methali za Kikorea. Jambo hili lahusika na fani katika methali. Tutajaribu mapigo hayo ya kimuziki au ridhimu katika methali yasiptee. Lililo muhimu zaidi katika somo letu ni yale maudhui na ujumbe, kwa hivyo tutazingatia upande wa maudhui kuliko wa fani.

Upungufu wa nafasi na wakati wa kutosha unatungima kuyaangalia mambo mengi yahusikayo na methali. Hayo ni kama vile mila, desturi, historia, imani, mambo ya kijadi, falsafa na kadhalika katika jamii ya Wakorea na ya Waswahili.

1.5. Msingi wa kinadharia

Njia rahisi ya kuziainisha methali ni kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti. Vitabu vingi vilivyoandikwa kuhusu methali ni vitabu ambavyo methali zimepangwa kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti. Mara nyingi kazi yoyote ile ya namna hii hubaki katika kiwango cha kuzikusanya methali na kueleza maana na matumizi yake.

Lakini udhaifu unaojitokeza katika unainishaji wa methali kwa kutumia mapangilio wa kialfabeti ni kwamba methali zenye kufanana kimaana hazina maumbo yaliyo sawa. Kuhusiana na udhaifu huo Albert Scheven (1981) anatueleza hivi;

Methali nyingi zimepangwa kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti. Kwa hakika njia hii ni njia rahisi zaidi kuliko njia nyingine zozote. Walakini methali, hasa methali za Kiswahili hazina umbo moja kila wakati. Fauka ya hayo, kila methali yenye kufanana kimaana na kimatumizi haianzi na neno moja tu. Hata njeo na nafsi hubadilika (4) (tafsiri yetu).

Kama mifano ya kuthibitisha maelezo yake tutatoa baadhi ya methali ambazo zakaribiana na kufanana kimaana na kimatumizi, lakini zinatolewa kwa namna zaidi ya moja zikiwa na maneno tofauti kidogo;

- . Cha kuvunda hakina ubani.
- . La kuvunda halina ubani.

- . Risifuye mvua imemnyea.
- . Alisifuye jua limemwangaza.

- . Hasira ya mkizi furaha ya muuvi.
- . Hasira za mkizi tijara ya muuvi.
- . Ana hasira za mkizi.

- . Dawa ya moto ni moto.
- . Sumu ya neno ni neno.

- . Mwenda mbio hujikwaa dole.
- . Mwenda haraka hukwaa dole.
- . Mwenda pole hujikwai.
- . Mwenda pole haumii miguu.
- . Mwenda pole hufika mbali.

- . Maneno mengi maradhi.
- . Maneno mengi uele.
- . Maneno mengi ukongo.
- . Maneno mengi hula akili.

- . Jitihadi haiondoi kuduru.
- . Jitihadi haiondoi amri ya Mungu.
- . Jitihadi na bidii haziondoi makadara.
- . Jitihada ya binadamu haishindi kudura ya Mungu.

. Juhudi haishindi kudura.

. Penye nia ipo njia.

. penye nia pana njia.

. Penye nia ndipo njia.

. Iwapo nia, njia hupatikana.

. Hakuna chanzo kisicho na mwisho.

. Kila chenye mwanzo kina mwisho wake.

. Lenye mwanzo lina mwisho.

. Hakuna mwanzo usiokuwa na mwisho.

Kama tuliyoangalia hapo juu, uainishaji wa methali kwa mpangilio wa kialfabeti unatutaliza tunapojaribu kuangilia yaliyomo na ujumbe.

Dilevile ni vigumu na hata haiwezekani kamwe kuziainisha methali kimaudhui kwa kuwa methali moja inaweza kutumiwa katika hali tofauti na miktadha mbalimbali iwe na maana tofauti kabisa. Inamaanisha tukiweka methali fulani kwenye kikundi maalum cha maudhui kutokana na uamuzi wetu ama maoni yetu, kuna maelekeo ambayo wengineo wenye maoni tofauti hawangekubaliana nasi.

Kwa mfano wakiambiwa methali hii ya Kikorea "Mitemo kumi inauangusha mti wowote," baadhi ya watu watafahamu kwamba yeyote ashawishiwaye mara nyingi, hata akiwa na moyo mgumu, nia

yake itabadilika. Wengine wangepasiri kwamba juhudi zisizokoma zinaliwezesha lisilowezezana kwa juhudi za kawaida.

Hata nadharia hiyo ingekuwa na udhaifu wake, tutatumia nadharia ya Albert Scheven (1981) ambayo inayazingatia maudhui yaliyomo katika methali. Imani yetu ni kwamba nadharia isiwe na marudio tu, bali iwe ni mwongozo na kwamba nadharia hiyo itosheleze lengo la somo letu ambalo halishughulikii umbo na fani ya methali, bali lashughulikia yaliyomo katika methali, yaani uketo wa kifalsafa na ujumbe.

Kutokana na uainishaji wa methali kimaudhui uliofanywa na Albert Scheven (1981), tuko na vikundi vifuataavyo vya aina za methali;

- 1) Matusi
- 2) Kuwa macho
- 3) Tamaa ya kuendeleza na kukuza mali
- 4) Hasira
- 5) Sura na urembo
- 6) Tendo la kushirikiana
- 7) Mwazimo
- 8) Uwezekano na kuchukuana na kupatana
- 9) Matokeo
- 10) Kuendelea bila kubadilika
- 11) Kushauriana
- 12) Ridhaa
- 13) Ushirikiano

- 14) Ujanja
- 15) Kifo
- 16) Maamuzi
- 17) Kungwa pombe
- 18) Wajibu
- 19) Maovu
- 20) Ubora
- 21) Tajiriba
- 22) Maaialiwa
- 23) Woga
- 24) Ujinga na werevu
- 25) Uhuru
- 26) Urafiki
- 27) Zawadi
- 28) Mungu na dini
- 29) Shukrani
- 30) Uchoyo
- 31) Afya na maradhi
- 32) Takirima
- 33) Njaa
- 34) Haraka
- 35) Unafiki
- 36) Hisani
- 37) Elimu
- 38) Mapenzi
- 39) Urongo
- 40) Adabu

- 41) Bwana na hadimu
- 42) Bahati mbaya
- 43) Wazazi na watoto
- 44) Umaskini na utajiri
- 45) Fahari na unyenyekevu
- 46) Tahadhari
- 47) Sifa
- 48) Siri
- 49) Maneno na unyamavu
- 50) Wizi
- 51) Kufaulu na kutofaulu
- 52) Iktisadi na ubadhirifu
- 53) Vita na amani
- 54) Wanawake na wanaume
- 55) Kazi na uvivu
- 56) Malimwengu na ulimwengu

Katika tasnifu yetu tutaongeza baadhi ya maudhui ambayo hayako katika uainishaji wa Albert Scheven na kuyaacha baadhi ya maudhui ambayo yamo katika uainishaji wake. Baadhi ya maudhui yanahusiana na hivyo basi hayo yatashughulikiwa pamoja.

1.6. Yaliyoandikwa kuhusu somo hili

Ili kuziangalia kazi mbalimbali zilizofanywa kuhusu methali yafaa kuyagawanya yaliyoandikwa kuhusu methali za Kikorea.

Lee, Ki Moon (1962) anadai kwamba neno halisi la lugha ya Kikorea ambalo lamaanisha methali halikuwa tangu zamani.(5) Amezipanga methali za Kikorea zipatazo 7,200 kwa kutumia mpangilio wa kifabeti. Kwa kuwa methali zimetumiwa katika kazi ya kifasihi anaonyesha sehemu fulani za kazi za kifasihi zenye matumizi ya methali. Ameeleza maana za methali na kuongesha methali zifananazo kimaana zinazotumiwa katika muktadha sawa. Dilevile amezifafanua methali zenye asili ya Kichina na methali za Kikorea zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kichina. Katika kazi yake anadhihirisha kwamba si rahisi kuzifasiri maana za methali kikamilifu. Ingawa amejaribu kuzieleza maana za methali amekosa kuzikosa methali zenye mawazo ya kimwinyi na yaliyomo yasiyo ya kimaadili. Piya ameangalia upande wa maana na matumizi ya methali, hakushughulikia upande wa fani na mtindo katika methali.

Ha, Tae Hung (1958) amezitafsiri methali za Kikorea kwa Kiingereza neno kwa neno na kuzifafanua methali zisizofahamika moja kwa moja. Mbinu inayotumiwa kuzipanga methali katika kazi yake yatofautiana na mbinu nyingine za kawaida. Limaanishalo ni kwamba amezipanga methali kwa mpangilio wa maneno yanayotumiwa katika methali. Kwa mfano methali zote za Kikorea zinazotaja neno 'ng'ombe' zimewekwa katika mahali pamoja. Lengo kubwa la kazi yake lilikuwa kuwafahamisha wageni kuhusu utamaduni wa Wakorea. Hakushughulikia upande wa maudhui na wa fani ila alizitafsiri methali za Kikorea kwa lugha ya Kiingereza na kuongeza maana na matumizi ya methali hizo.

Chung, chong Hwa (1991) amezilinganisha methali za Kikorea na za Kiingereza. Amezianisha methali kimaudhui na kuziweka methali hizo katika vijikundi themanini kufuatana na maudhui. Anasema kwamba lengo la kuhariri Kamusi ya Methali za Kikorea-Kiingereza ni kuangalia kufanana na kutofautiana kwa utamaduni wa Wakorea na wa Waingereza. Katika mbinu yake ya kuzianisha methali kimaudhui hadhihirishi nadharia iliyomnufaisha na kutumiwa katika kazi yake.

Katika kitabu chake Kamusi Kuu ya Methali za Kikorea, Song, Jae Son (1983) amezikusanya methali za Kikorea zipatazo 25,000 na kuzipanga methali hizo kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti. Anaeleza kwamba methali 18,000 zina asili ya Kikorea na zingine 7,000 zinaainishwa kuwa methali zenye asili ya Kichina. Akitoa matumaini anasema;

Korea ni nchi yenye historia ndefu ya miaka elfu tano na nchi ambayo wananchi wanajionea fahari kubwa utamaduni wao unaoimarika. Kwa hivyo tuna furaha ya kuwa na urithi wa utamaduni wa kijadi ambao ni kama hazina. Methali hali kadhalika ni aina moja ya utamaduni huo.

Baada ya kupata uhuru, utamaduni wa Kimagharibi umeingia fikrani mwa vijana wa kizazi hiki kama mawimbi ya baharini mpaka utamaduni wa kitaifa ukadidimia.

Matumaini yetu ni kwamba kazi hii ishubiane na vijana na wananchi wenye kutaka kujua utamaduni wa kitaifa. (6)

Kamusi hii inachukuliwa kuwa kazi kubwa tena muhimu kuliko zote katika utafiti wa methali za Kikorea. Ingawaje ni kazi kubwa isiyo

na kifani katika idadi nyingi za methali, maelezo ya kutosha kuhusu maana na matumizi ya methali hizo hayapatikani katika kazi yake. Mathalani methali nyingi huwa na maana zaidi ya moja, kwa hivyo ni muhimu kuzieleza maana hizo mbalimbali ambazo zafahamika na kutumika kwa namna mbalimbali.

Katika kitabu cha A Dictionary of Swahili-English-Korean Proverbs Kineene wa Mutiso na Yang, Chul Joon (1988) wanazilinganisha methali za Kiswahili, Kiingereza na Kikorea kwa kutumia mbinu ya kuziweka methali za jamii hizo tatu zinazofanana kimaana. Ni kazi ya kwanza katika kuzilinganisha methali za jamii hizo tatu, lakini baadhi ya methali zimepangwa katika vijikundi vya kimaudhui visivyohusiana na maswala yanayojitokeza katika methali hizo.

Tukiangalia upande wa methali za Kiswahili, kazi nyingi zimefanywa kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti. Albert Scheven (1981) amezitafsiri methali za Kiswahili kwa lugha ya kiingereza na kuzipanga methali hizo kwa mpangilio wa kimaudhui. Amevitenga vijikundi hamsini na sita vya maudhui na kuzipanga methali chini ya kila kijikundi cha maudhui. Ameeleza maneno magumu katika methali na kufasiri matumizi ya methali. Dilevile ameziongeza methali zinazofanana kimaana na methali za jamii nyingine, hasa za Kiingereza ili kuwawezesha wasomaji kufahamu kwa urahisi. Kazi yake haishughulikii fani na maumbo ya methali. Ijapokuwa haangalii upande wa fani, kitabu chake Swahili Proverbs Nia zikiwa moja, kilicho mbali huja ni kazi muhimu sana iliyofungua ukurasa mpya katika utafiti wa methali za Kiswahili.

Katika tasnifu yake Uhakiki wa "Nthimo (Methali)" za Kikamba Geoffry Kitula King'ei (1982) amehakiki maswala kadha wa kadha yanayoibuka katika uchunguzi wa methali. Maswala hayo ni kama vile chimbuko la methali, mtindo na sifa mbalimbali za kifasihi na kiisimu katika methali, kazi na matumizi ya methali na kadhalika. Ili kuwapatia wasomaji msingi ya kuzifahamu methali za Kikamba, anatoa maelezo kuhusu mambo kadha wa kadha yaliyo muhimu katika jamii ya Wakamba. Maelezo ya mambo hayo kwa muhtasari yahusu historia, utamaduni, mila, ada mbalimbali na kadhalika katika jamii ya Wakamba. Udhaifu wa kazi hii ni kwamba amejaribu kuyaangalia mambo mengi, hivyo anakosa kuyaangalia kwa undani na upana.

Kazi ya S. Karama na M. Saidi (1983) ni Maelezo ya Methali za Kiswahili. Wamezikusanya methali za Kiswahili katika janibu mbalimbali za pwani ya Kenya na Tanzania. Wamezipanga methali hizo kwa kutumia mpangilio wa kialfabeti na kuongeza maana na matumizi. Kama kazi nyingi zilizofanywa kuhusu methali za Kiswahili kazi hii imebaki katika kiwango cha kuzikusanya methali na kueleza maana na matumizi bila kuzihakiki.

1.7. Njia za utafiti

Kama tanzu nyinginezo za fasihi simulizi kama vile ngano, hadithi, hurafa, vitendawili, nyimbo na kadhalika zinavyopokezanwa kizazi kwa kizazi kwa njia ya kusimuliana ndivyo ambavyo methali huhifadhiwa kuwa na uhai na nafasi yake katika jamii. Kwa sababu hii

watafiti wa fasihi simulizi wasipozingatia umuhimu wa masimulizi au mazungumzo ya watu na kutegemea vitabu na kongoo za kitaaluma tu, watakwama katika utafiti wao wa methali.

Katika utafiti wetu hatutategemea vitabu au makala tu, bali tutatumia methali za siku hizi ambazo hazimo kwenye kamusi na makala. Hatutasitasita kutembelea sokoni, barabarani, kazini na mahali penginepo panapohitajika kwa kusudi la kukusanya methali hai za maisha. Dilevile kumekuwa na makala nyingi ambazo zashughulikia methali katika magazeti mbalimbali. Bila ya shaka, makala hizo zitakusanywa na kuchambuliwa katika utafiti wetu.

Fauka ya hayo, tutarejelea mehali ambazo zimeathiriana na methali za Kiswahili na za Kikorea. Mara nyingi methali hushika mizizi imara zaidi kwa mawasiliano kati ya tamaduni mbalimbali zinazotofautiana. Tukitoa methali za Kikorea kwa mfano methali nyingi za Kichina zimeingia kwenye methali za Kikorea na zikawa za Kikorea kindakindaki. Hapana shaka yoyote kwamba methali hizo za Kichina zimerutubisha na kuziimarisha methali za Kikorea. Yeyote asisitizaye methali za Kikorea zenye asili ya Kichina zisichukuliwe kama za Kikorea apaswa kuuzingatia uhalisi uliopo wa kwamba hakuna utamaduni wowote usioingiliana na tamaduni zinginezo.

Tutatafsiri methali za Kikorea (*Sokdam*) kwa Kiswahili sanifu. Tutakapotafsiri methali za Kikorea tutajaribu kutafsiri neno kwa neno zisipoteze maana sahihi iliyo muhimu sana kufahamu utamu wa lugha na sifa za methali kwa ujumla. Dilevile hatutakosa kueleza baadhi ya

maneno yasiyofahamika katika lugha ya Kiswahili ili tafsiri yenyewe idhihirike kimaana. Maneno haya hutokana na tofauti za kimazingira na za kiutamaduni.

Isitoshe maelezo mapana kuhusu utamaduni wa Wakorea kwa ujumla yatatolewa kila mahali panapohitajika kwa sababu methali ni zao na utamaduni.

Ili kuitekeleza kazi ipasavyo tutatumia maktaba za vyuo vikuu mbalimbali nchini Kenya na Tanzania ili kupata maandishi mengi iwezekanavyo kuhusu methali. Waaidha itatubidi kuwa wasikilizaji ambao wako tayari kukusanya methali kutoka kwa masimulizi au mazungumzo ya umma ambayo ndiyo chemchemi ya fasihi simulizi ikiwemo methali.

Ubalozi wa Jamhuri ya Korea (Korea Kusini) nchini Kenya ni mahali panapofaa kwa uchunguzi wa mambo mbalimbali yahasuyo utamaduni, historia, mila na kadhalika. Tutapekua makala mengi iwezekanavyo ili kutimiza malengo ya utafiti wetu.

SURA YA KWANZA

Tanbihi

1. Khamis, Said A. (1983), **Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Kitanzania** katika Mulika Na. 15,

Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa
Kiswahili. Uk.3.

2. Oliver, Roland and Mathew, Gervase (1963), **History of East
Africa Vol 1**, London: Oxford University Press.

Uk. 107-108.

3. Kim, Dae Jung (1984), **Nyaraka za Kim Dae Jung kutoka
Gerezani-Nikikumbatia Huzuni ya Kitaifa**,

Seoul: Chongsa Publishing Co. Uk. 223.

4. Scheven, Albert (1981), **Swahili Proverbs Nia zikiwa moja,
kilicho mbali huja**, Washington: University

Press of America, Inc. Uk. 80.

Anaendelea kusema kwamba "Niliamua kuzipanga methali kimaudhui na kuongozwa kwa kiasi fulani na mbinu ya Northcote W. Thomas aliyezipanga methali za *Iba*, mbinu ambayo ina manufaa dhahiri. Hata hivyo, kwa upande mwingine ni vigumu na haiwezekani kuziweka methali kwenye kundi fulani linaloweza kukubaliwa na wote kwa sababu methali moja inaweza kutumiwa katika hali tofauti na hivyo methali hiyo ingeweza kuwekwa chini ya kundi zaidi ya moja la kimaudhui. Zadi ya hayo, si rahisi kila mara kubainisha kati ya maneno halisi yenyewe na maana za kawaida."

5. Lee, Ki Moon (1962), **Kamusi ya Methali za Kikorea**, Seoul:

Il Jo Gak Publishing Co. Uk. viii.

Releza kwamba neno *Sokdam* lilianza kutumiwa
kwa upana katika lugha ya Kikorea kuanzia
karne ya 18.

6. Song, Jae Son (1983), **Kamusi Kuu ya Methali za Kikorea**,

Seoul: Somundang Publications Ltd. Uk. 2.

SURA YA PILI

2.0. UTANGULIZI

Binadamu wanaishi katika mazingira mbalimbali ambayo yanayaathiri maisha ya kila siku ya binadamu. Maathiriano hayo baina ya binadamu na mazingira hushika mzizi imara katika utamaduni.

Lugha vilevile hupata uhai na kubadilika katika uhusiano huo kati ya binadamu na mazingira yanayowazingira binadamu hao. Tukichukua Waeskimo wanaoishi karibu na Bahari ya Aktiki na Kisiwa cha Greenland kama mfano wa kueleza uhusiano uliopo kati ya mazingira na matumizi ya lugha, tunaona kwamba watu hao wana msamiati mwingi unaomaanisha theluji na barafu na kwamba wanaainisha maneno yamaanishayo theluji na barafu katika hali mbalimbali. (1)

Ingawa lengo kubwa la lugha kwa ujumla ni mawasiliano miongoni mwa wanajamii, lugha za binadamu huwa na sura mbalimbali zinazotofautiana kulingana na mazingira yao.

Methali kama fasihi simulizi hutumia lugha kama mali-ghafi, kwa hivyo taswira mbalimbali za mazingira na vyumbe hutiririka katika methali, twaweza kudai kwamba methali zinaweza kulinganishwa kama kioo cha kutazamia mazingira maalum na utamaduni ambo unaumbwa katika mazingira hayo kama kitovu. Mazingira hayo yanatofautiana kijiografia na tofauti hizo kimazingira husababisha tamaduni zenye sura na sifa mbalimbali. Kwa hivyo ufahamu wa

mazingira hayo unatupatia nafasi na uwezo wa kuangalia utamaduni methali kama fasihi simulizi zikiwemo.

Hivyo basi endapo tutakosa kuziangalia taswira hizo mbalimbali za mazingira na viumbe zinazosawiriwa katika methali na tanzu nyinginezo za utamaduni hatutaweza kuzielewa wala kuzifahamu kwa undani zile falsafa nzito za methali zinazoundwa katika mazingira maalum.

Hata ingawa hisia za binadamu za kiulimwengu zinafanana kimsingi, namna ambavyo wanajamii wanaonyesha hisia hizo katika maisha yao hutofautiana kufuatana na miktadha mbalimbali ya kiutamaduni na kimazingira. Kwa mfano tukikutana na marafiki au wanaaila wenge uhusiano na umbuya mzuri huwa tunasalimiana kwa furaha. Ingawa ile hisia ya furaha inafanana, ule mtindo wa kusalimiana huwa unahitilafiana katika jamii mbalimbali. Katika nchi nyingi za Mashariki ya Mbali watu wanasalmiana kwa kuinamisha vichwa vyao kama ishara ya heshima.

Kufuatana na maelezo ya Lee, Kyu Tae (1987) watu ambao wanajishughulisha na kazi za uwindaji, ufugaji na biashara wanalazimika kuhama na kuhamia hapa na pale kwa sababu ya kazi zao. Kwa kawaida watu wa namna hii hawasalimiani kwa kuinamisha vichwa vyao, bali wanapeana maamkizi bila kuinamisha kichwa.(2) Bila shaka kule kutofautiana katika mtindo wa kupeana maamkizi kunasababishwa na tofauti za kimazingira na kiutamaduni.

Katika uundaji wa methali yoyote ile viumbe mbalimbali vilivyoko katika mazingira kama vile wanyama, wadudu, mimea, miti na kadhalika husawiriwa kuwa na sifa zinazofanana na za kibinadamu. Watu huwa wanavipatia viumbe hivyo sifa maalum. Mara nyingi sifa hizo kuhusu kiumbe maalum hufanana kwa kuwa binadamu huangalia tabia ama sura ya kiumbe hicho kwa uangalifu na makini katika maisha yao na hisia zile zinazohisika kwa kuangalia au kuingiliana nazo zinakuwa sawa.

Zile taswira za viumbe, mazingira na halia za kimaumbile ni dhihirisho ambalo linatuonyesha picha halisi ya jinsi wanajamii fulani wanavyoingiliana na kuathiriana na mazingira yanayowazingira katika mazingira yao. Katika sura hii tutajishughulisha na taswira hizo katika viwango mbalimbali.

Kwanza, tutajaribu kuyaangalia mambo yanayojitokeza kuhusiana na taswira hizo. Hayo ni kama ibada, miiko na ushirikina. Ingawa mambo haya yamefifia katika karne hii kwa sababu ya maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia bado yanachukua nafasi muhimu katika kufahamu umbo asilia la fikira na imani za watu.

Pili, mambo tutakayotaribu ni tamathali za usemi zinazotumiwa kuzisawiri taswira hizo. Hili ni swala la mbinu ya kutiririsha hisia, mawazo, falsafa na mafunzo ndani ya methali.

Katika sehemu ya tatu tutaziangalia taswira hizo zinazosawiriwa katika methali za Kikorea na za Kiswahili. Kwa kuwa taswira ya

kiumbe fulani ingeonyeshwa ikiwa na sifa zinazokinzana tutaangalia sifa kwa ujumla, halafu tutaangalia sifa zinazokinzana kwa kuzichukua methali kadha wa kadha. Isitoshe tutarejelea vitabu mbalimbali ambavyo vinatuonyesha taswira za viumbe, mazingira, halia za kimaumbile na mengineyo.

2.1. Ibada, miiko na ushirikina katika taswira za viumbe

Historia ya binadamu imekuwa na harakati zisizokuwa na kikomo dhidi ya mazingira. Zamani za kale watu hawakujiweza kwenye hali zenye maafa na maangamizo yaliyosababishwa na maumbile. Wanadamu walitishika na nguvu za ajabu zilizosababisha mambo yatukie. Halia za kimaumbile ambazo binadamu walishindwa kuzifumbua ziliwafanya watu waamini kuna Mungu au nguvu inayotawala utaratibu wa ulimwengu. Dilevile walianza kuamini kwamba kila kiumbe kinahulukiwa na roho.

Mara kwa mara imani hii huchukuliwa kama chimbuko la dini katika umbo la kimsingi. Imani ya namna hii huitwa *totemism* kwa Kiingereza. *Totemism* hujadiliwa kuwa namna moja ya dini ambayo hujumuisha imani, ibada kwa wanyama.

Dilevile watu wa jamii fulani wanajinasibisha na wanyama fulani na kuabudu kama nguzo ya ibada. Kujinasibisha huko huwatolea wanajamii mwiko au onyo maalum wasifanye jambo au kitendo fulani kuhusiana na wanyama hao.

Kwa mfano Waghana waongea lugha ya *Kilshi* katika Afrika Magharibi wanagawanyika katika makundi kumi na mawili ya kinasaba. Makundi hayo ni chui, nyati, mbwa, kasuku, mgomba, mhindi, mtumwa, udongo mwekundu, mnazi, *Abdazi* na *Dumna* au *Dwimina*. Chui huabudiwa kama wanyama watakatifu na watu wa nasaba ya chui. Mtu yeyote katika nasaba hiyo haruhusiwi kuwawinda chui na iwapo amemwinda chui kwa makosa bila kukusudia kumwua inambidi kupaliza sauti "Nimemwua ndugu yangu" na kuweka mafuta ya nazi kwenge jeraha. Iwapo maiti ya chui italetwa katika kijiji, wanakijiji wenye kujinasibisha na chui lazima waipake chokaa kama alama ya maombolezo na kuizika. Pamoja na hayo waonapo chui aliyekufa lazima watapanye vipande vya kitambaa cheupe juu ya maiti na kupaka mafuta ya nazi juu ya pua na mdomo wa mnyama huyo ili kuongesha heshima na huzuni. Endapo mwenye nasaba hiyo ya chui anasadifu kukutana na chui safarini yampasa kurudi kwo. (3)

Hali kadhalika Wakorea wanajinasibisha na dubu. Katika hurafa inayohusu kuanzishwa kwa taifa la Wakorea mwana wa Mungu wa Peponi alitamani kuteremka kwenge ulimwengu huu ili awanufaishe watu wote. Aliteremka kutoka Peponi kuja ulimwengu huu akibeba upepo, mvua na mawingu. Wakati huo huo kulikuwa na dubu na chui wa Bara Hindi ambao walitaka kuwa binadamu. Walitiwa majaribioni ili wawe wanadamu. Iliwalazimu kukaa pangoni wakila kitunguu saumu na pakanga kwa siku mia moja. Dubu alifanikiwa kuvumilia hali hiyo na akahulukiwa kama binadamu. Lakini yule chui wa Bara Hindi hakuweza kutimiza masharti hayo yaliyotolewa na mwana wa Mungu wa Peponi.

Kwa sababu ya kutoweza kuvumilia hakuweza kuwa binadamu, bali alibaki kama aina moja ya mnyama. (4)

Kama tunavyoona katika taswira zao dubu anasawiriwa kama kiumbe chenye uvumilivu, lakini taswira ya chui wa Bara Hindi ni kingume cha dubu. Maoni haya yanadhihirishwa na F.J. Seligson (1986) anayeeleza kwamba;

Dubu ni muumilivu kama walivyo wanawake wa Kikorea, lakini aweza kughadhibika vilevile kama wanavyoweza wanawake wa Kikorea. (5)

Kama tulivyotangulia kutaja umuhimu wa hurafa ya *Tangun* inatujulisha jinsi Wakorea walivyofikiria kuhusu mambo kadha wa kadha yaliyowazingira. Ingawa Wakorea wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na dini za kigeni kama vile Ubudha, Ukonfusiasi (Confucianism), Utao (Taoism), Ukristo na imani na mawazo mengineyo, Ushamani (shamanism) umeshika mizizi imara fikirani mwa Wakorea. Kufuatana na imani hiyo majabali, milima, mito, miti na vinginevyo huwa na nguvu za ajabu na roho.

Kwa hivyo penye majabali, miti, mito na milima paliabudiwa kama patakatifu au mizimu. Wakorea waliamini kwamba vitu hivi vilikuwa na nguvu zistaajibishazo za kuliwezezasha lisilowezekana kwa nguvu za watu wa kawaida.

Kama tulivyotangulia kuiangalia hurufa ya *Tangun*, Wakorea wanajinasibisha na dubu na kumtukuza kama mnyama wa *Totem*.

Katika hurafa ya *Tangun* dubu anajitokeza kama auumiliaye dhiki na machungu ya kila namna ili astahili kuwa binadamu. Taswira ya dubu katika hurafa higo ni ustahamilivu. Licha ya taswira higo dubu huwa anawakilisha sifa za ujinga, upumbavu, upungufu wa akili katika methali nyingi za Kikorea. Tukitoa methali mbili za Kikorea kwa mfano;

1. Ni mpumbavu kama dubu.

2. Achezaye sarakasi ni dubu na apokeaye fedha ni

Mmanchu

m.z. Hapa dubu ni ajitahidiye na *Mmanchu* aliye mwenye dubu huyu anafaidika kwa jasho la dubu. Kwa sababu ya upumbavu wake anadhulumwa na kunyonywa na *Mmanchu*.

Chui wa Bara Hindi anayesawiriwa kama mnyama asiye na uumilivu anajitokeza mara nyingi katika methali za Kikorea zenye taswira za chui wa Bara Hindi.

3. Hata chui wa Bara Hindi hali uchengelele wa mwenye wake wawili.

4. Ajaribuye kumwepuka ibilisi hukutana na chui wa Bara Hindi.

5. Waweza kumdanganya chui wa Bara Hindi anayekuja kutoka nyuma, lakini huwezi kuyadanganya majaaliwa yanayokujia kutoka mbele.

6. Mbwa aingiliwaye na wazimu humkamata chui wa Bara Hindi.

7. Kaa wa baharini hajui ukali wa chui wa Bara Hindi.

8. Chui wa Bara Hindi anayesikia njaa hamtambui ofisa.

9. Anatafuta nyushi za chui wa Bara Hindi aliye hai.

10. Ni chui wa Bara Hindi wakati wa alfajiri.

m.z. Kwa kawaida chui wa Bara Hindi huingia kwenye mashamba na vijiji ambapo watu wanakaa ili atafute kitu cha kula wakati wa usiku, halafu anarudi mlimani wakati panapopambazuka. Ingawa chui wa Bara Hindi anapewa jina la mfalme wa wanyama wote kwa ajili ya ukali, uhodari na nguvu zake hawezi kuonyesha sifa hizo kweupe.

11. Mgeni akutembeleaye miezi ya Mei na Juni hukutisha zaidi kuliko chui wa Bara Hindi.

m.z. Watu wa Mashariki ya Mbali walitumia kalenda iliyotengenezwa kulingana na mwenendo wa mwezi

(lunar calendar). Mwezi wa mei katika kalenda ya kimwezi huwa wa Juni katika kalenda ya kijua (solar calendar). Wakati huo ni wakati ambapo watu husikia Joto na unyevu. Kwa sababu hii ni vigumu kumkaribisha mgeni. Katika methali hii chui wa Bara Hindi anatumwa kuchorea hali ya kutisha.

12. Anatia mduko katika pua la chui wa Bara Hindi anayelala.

13. Chui wa Bara Hindi anayesikia njaa anakula hata towash.

14. Bila kujasiri kuingia ndani ya pango la chui wa Bara Hindi huwezi kumkamata hata mtoto wake.

15. Ni hadithi ya wakati chui wa Bara Hindi alipovuta sigara.

m.z. Katika methali hii chui wa Bara Hindi anapewa sifa kama walizo nazo binadamu. Kitendo hiki cha ajabu kinatokana na hadithi ya zamani.

16. Chui wa Bara Hindi hubakisha ngozi nzuri na binadamu hubakisha majina mazuri.

Katika methali nyingi za Kikorea taswira za chui wa Bara Hindi ni ukali, ujasiri na uhodari. Kingume cha taswira hizo za kuwatisha watu, pia anaonekana kuishi akisuhubiana na watu.

Ili kuangalia ushirikina katika taswira za wanyama ni muhimu sana kuliangalia chimbuko la ushirikina. Aghlabu ushirikina hubuniwa kuwahimiza wanajamii kutenda mema yenye maadili na adabu kama anavyodai I. Mbaabu (1985);

Ushirikina ni njia moja ambayo imefaulu sana kuhifadhi usalama. Waswahili kama jamii zinginezo wana ushirikina mwingi ambao unahusu mafunzo ya nyanja nyingi za maisha. Tusiisahau kwamba kuna watu wanaosema kwamba ushirikina unahusu mambo ya uwongo ambayo hayafai kuzingatwa. Dile tunavyojaribu kusisitiza ni kwamba baadhi ya imani hizi za ushirikina zina msingi wa ukweli, lengo na ukweli fulani maalum maishani. (6)

Baadhi ya methali ambazo zaweza kuthibitisha dai hili ni;

17. Ukipiga mruzi wakati wa usiku mwizi huja.

. A whistling maid boded never luck to a house.

(Methali ya Kiingereza)

taf. . Mwanamwali apigaye mbinja hakuibashiri bahati
njema nyumbani kamwe.

18. Ukikata kucha za vidole usiku mwizi huja.

. Kukata kucha usiku kunaleta ufakiri. (Methali ya Kiswahili)

. Kulimbika kucha ni ugonjwa wa kujitakia. (Methali ya Kiswahili)

Ingawa lengo kubwa la kubuni ushirikina ni kukataza wanajamii wasitende mambo maovu au mambo ambayo huchukuliwa kuwa hayastahili kufanywa, tunashuhudia baadhi ya imani za ushirikina zisizo na msingi maalum. Aghalabu imani hizi hutokana na sifa maalum wanazopewa na wanajamii.

Katika jamii ya Waswahili na Waafrika kwa ujumla bundi hujulikana kama ndege aletaye nuhusi ambapo hapana msingi maalum, ilhali ndege huyo husawiriwa kama mjinga au mtu ajisingiziaye na anayejifanya. Waswahili huamini kwamba bundi hubashiri kifo wanapoimba. Imani ya namna hii inaaminiwa kutokana na sura isiyopendeza na kilio kinachochukiza. Mara nyingi imani ya namna hii huambatana na uchawi. Tukiangalia imani hizo za ushirikina katika methali za Kiswahili;

. Bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo.

. Kuiga sauti ya bundi usiku ni kuwakaribisha siafu nyumbani.

Imani hizi za ushirikina huambatana na miiko. Divo hivo paka mweusi hudhaniwa kuwa ishara ya bahati mbaya na msiba. Methali inayoongesha imani hii ni;

. Kukutana na paka mweusi njiani ni bahati mbaya.

Ushirikina unaopenya katika jamii ya Wakorea ni kwamba kunguru waliapo huwa wanabashiri kifo. Wakorea humfikiria kunguru kuwa mjumbe wa kifo, hivyo basi anaporuka juu ya kijiji au nyumba zao, Wakorea hutabiri kifo cha mwanakijiji fulani. Tukitoa baadhi ya methali za Kikorea ka mfano;

19. Kilio cha kunguru hubashiri kifo.

20. Amekuwa chakula cha kunguru.

m.z. Wakorea huamini kwamba kunguru hula maiti za watu au makimba ya wanyama. Mtu anapofariki ulimwengu huzikwa. Yale mazishi hutofautiana katika mataifa mbalimbali. Wakorea wanaoamini dini ya Kibudha huichoma maiti mpaka inabaki majivu. Wale Wakorea wasio wafuasi wa dini ya Kibudha huiweka maiti ndani ya jeneza na kuizika kufuatana na mila na utaratibu maalum. Kwa hivyo methali hii inatufahamisha kwamba mtu fulani aliyeaga dunia anaachwa bila kuzikwa kwa kuwa hana wanaaila wala marafiki wanaoweza kuizika maiti hiyo.

21. Ni kama kunguru wanaoruka wakijumuika katika shamba lenye maiti ya farasi.

m.z. Methali hii hukaririwa hasa na Wakorea wanoishi katika kisiwa cha *Cheju* kilichoko kusini mwa Rasi ya Korea. Wanajeshi wa Mongolia walipovamia ufalme wa *Korya* mnamo karne ya 13 waliwafuga farasi wengi katika kisiwa cha *Cheju* kwa madhumuni ya kuivamia nchi ya Japan. (7) Hii imekuwa sababu ambayo kumekuwa na farasi wengi kisiwani huko. Methali moja inayosimulia ukweli huu wa kihistoria ni;

22. Anapozaliwa mtu apelekwe Seoul na anapozaliwa farasi apelekwe katika kisiwa cha *Cheju* Kwa vile vyovyote hapa pametajwa kunguru kama ndege anayekula maiti.

23. Kunguru katika ugonjwa.

m.z. Methali hii inafanana na methali ya methali ya Kiswahili, Hakuna msiba usio na mwenziwe. katika matumizi yake. Taswira ya kunguru katika methali hii huambatanishwa na sifa kama vile ubaya na msiba.

24. Aliapo kunguru panatukia msiba mkubwa.

Kama tuonavyo hapa watu huwa na taswira mbalimbali za viumbe na taswira hizo husababisha miiko, ushirikina na ibada katika maisha

yao. Taswira hizi zinapaswa kuangaliwa kwa namna mbalimbali ili tufahamu utamaduni fulani kwa undani.

2.2. Tamathali za usemi katika methali

Methali yaweza kuchukuliwa kuwa namna moja ya fasihi ambayo hushika mzizi wake katika utamaduni wa umma. Maudhui ya methali huwa mawazo na mafunzo mbalimbali yanayochujwa katika mazungumzo na maisha ya watu. Sifa moja ya methali ni ufupi. Hivyo basi sio rahisi kutiririsha mawazo na fikira zao kwa maneno mafupi, bali ni kazi ngumu inayohitaji ustadi wa kiwango cha juu katika uteuzi na matumizi ya maneno. Maneno hayo yangawa mafupi huwa yanawakilisha dhana mbalimbali ya falsafa nzito.

Tamathali za usemi katika methali ni mbinu moja ya kuongesha mawazo na fikira za watu kwa maneno mafupi ambayo huwa yanachukua taswira za viumbe mbalimbali. Kwa sababu hii tamathali za usemi zinazotumiwa katika methali hutuchorea taswira maalum za mazingira, viumbe na kadhalika.

Tamathali za usemi zinazotumiwa mara nyingi zaidi katika methali ni tashibiha, tashihisi au uhaishaji na sitiari. Mara kwa mara sitiari yenyewe hudhaniwa kuwa methali.

I. TASHIBIHA

Tamathali hii ni ulinganishaji wa vitu viwili au watu wawili au zaidi kwa kutumia maneno ya ulinganisho au viunganishi-linganishi

kama vile kama, fanana na, mithili, mithali ya, sawa na, kama kwamba, mfano wa, shabaha, shabaha ya, kana kwamba, na mengineyo ya aina hii ambayo inatumiwa kuvilinganisha watu au vitu viwili vilivyo bayana.

25. Asema kama kipofu anavyoeleza kuhusu umbo la ndovu.

m.z. Methali hii hutumiwa kwa mtu anayesema mengi kuhusu jambo fulani ambalo halijui au kwa mtu anayejifanya kulijua jambo fulani, ilhali hana habari wala tajiriba.

26. Yu kama mtu ajengaye ukuta dhidi ya soni.

m.z. Hapa ulimwengu kuna watu wasioona soni katika dhambi au makosa ambayo huwafedhehesha watu wa kawaida.

27. Anaonekana kama ndege bila mkia.

m.z. Katika methali hii ndege bila mkia huashiria mtu anayekosa sura nzuri na ukamilifu.

28. Ni kiasi kama machozi ya panya aliye mbele ya maiti ya paka.

m.z. Uhusiano kati ya paka na panya hulinganishwa na uhusiano wa maadhui au uhusiano usioweza kupatanishwa. Kwa hivyo machozi ya panya ni unafiki. Vilevile machozi yanayomtoka panya ni kiasi

kidogo kabisa. Mara nyingi methali hii hutumiwa kumaanisha kiasi kidogo na unafiki.

29. Ni kama chura anayeishi ndani ya kisima.

m.z. Sehemu ambayo unaweza kuitazama kutoka ndani ya kisima ni sehemu ndogo tu ya mbinguni. Chura yule angedai sehemu hiyo ndogo ni ulimwengu mzima. Katika matumizi halisi methali hii inatumiwa kumsawiri mtu ambaye ana maarifa machache au amefingika katika malimwengu au mambo ya dunia.

Tukiangalia matumizi ya tamathali hii katika methali za Kiswahili;

- . Mtu na rafikiye ni kama kombe, haziachi kuchakacha.
- . Kulingana kama kupe na mkia wa ng'ombe.
- . Ni kama nguvu ya mayonda, zitakwishilia nyangwani.

II. TASHIHISI (UHAISHAJI)

Katika tamathali hii wanyama au vitu hupewa sifa za binadamu.

Tukitoa methali ya Kiswahili kwa mfano;

- . Samaki akilia machozi yake yapelekwa kwa maji.

Kulia ni kitendo cha binadamu ambacho kinaongesha huzuni au furaha isiyo na kifani. Lakini methali hii inahusu machozi yasiyo na maana na samaki anasawiriwa kama binadamu.

Msingi wa tamathali hii huwa hadithi simulizi na hali kadhalika binadamu anahayawanishwa kwa sababu ya tabia maalum. Lakini anapohayawanishwa kutokana na tabia au sifa maalum tamathali ya tashibiha hutumiwa.

Ifuatayo ni mifano inayoongesha tamathali ya tishihisi au uhaishaji katika methali za Kiswahili;

- . Ndege mjanja hunaswa na tundu bouu.
- . Ng'ombe hajui thamani ya mkia wake mpaka umekatwa.
- . Kunguru mwoga hukimbiza bawa lake.
- . Hasira ya mkizi furaha ya muuvi.
- . Ahsante ya punda ni teke.

Kwa sababu gani wanamsawiri punda kama mwenye utovu wa shukrani? Sifa wanyama wanazopewa huwa zinatokana na hadithi au tabia za wanyama hao.

Methali za Kikorea zenye matumizi ya tamathali hii ni nyingi kama zinavyoorodeshwa hapa chini;

30. Chura hafikiri wakati alipokuwa kiluwilwi.

m.z. Watu wakitajirika hawafikiri wakati walipokuwa maskini. Methali hii hutumiwa kumkosoa au kumdhihaki mtu ambaye anaringa kwa utajiri au cheo chake bila kujikumbusha wakati wake wa dhiki na matatizo.

31. Nguruwe aliyechafuka kwa makapi humkashifu
nguruwe aliyechafuka kwa mavi.

m.z. Kuchafuka kwa makapi kunafanana na kuchafuka kwa mavi katika uchafu wake. Mtu mwenye dosari anapomkosoa mwingine methali hii hutumiwa.

III. SITIARI

Kutofautiana na matumizi ya tamathali ya tashibiha viunganishi-linganishi au maneno ya ulinganisho hayatumiwi. Tamathali hii hutumika katika mashairi na methali kwa kuwa ishara na isitiara hutumiwa sana katika tanzu hizi mbili ili kuwakilisha dhana dhahania. Zaidi ya hayo mashairi, hasa mshororo fulani hutumiwa kuwa methali katika maisha ya watu na hali kadhalika methali zinazotumiwa katika maisha ya binadamu hukaririwa katika mashairi.

Kwa mfano mishororo mingi katika mashairi ya Muyaka hupatikana katika methali za Kiswahili. Tukiangalia shairi moja la Muyaka;

Dunia mti mkavu, kiumbe siulemele,
 Ukaufangia nguvu kuudhabiti kwa ndole,
 Mtiwe ni mtakavu, mara ulikwangushile.
 Usione kwenda mbele, kurudi nyuma si kazi.

Dunia mwendo wa ngisi, kamwe msililiwale,
 Mkakithiri utesi kwenda mwenendo wa kule;
 Na kutupiza viasi kwa hayano na hayale,
 Usione kwenda mbele, nyuma si kazi.

Dunia kitu dhaifu, kiumbe sijetele,
 Kwa kupata utukufu na furaha ya milele;
 Kumbuka na uvundifu ujapo ni kama ndwele;
 Usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi.

Mishororo ya kwanza na mwisho katika kila ubeti wa shairi hili hutumika mara nyingi kama methali. Dunia haina uhusiano wa moja kwa moja na mti mkavu, mwendo wa ngisi wala kitu dhaifu. Wanaposema Dunia mwendo wa ngisi huwa wanaashiria sifa maalum za dunia ambazo zingehusishwa na mwendo wa ngisi. Aghalabu sifa hizo huweza kuwa ni kutowezekana kwa kuelewa mwenendo wa dunia au kutotabirika kwa mambo yatayotukia.

Methali zenye tamathali hii hupatikana kwa wingi katika methali za Kikorea na za Kiswahili. Hizo kwa upande wa methali za Kiswahili ni zifuatazo;

- . Akili ni mali.
- . Hasira ni hasara.
- . Dawa ya moto ni moto.
- . Mtoto wa nyoka ni nyoka.
- . Ahadi ni deni.
- . Ajizi ni nyumba ya njaa.
- . Sumu ya neno ni neno.
- . Ujana ni moshi, ukienda haurudi.
- . Subira ni ufunguo wa heri.
- . Majuto ni mjukuu.

Kwa upande wa methali za Kikorea tunaona ishara na istiara zinatumiwa sana kuwakilisha dhana au kitu fulani. Kwa mfano yungiyungi la Kihindi ni ishara ya dini ya Kibudha katika fasihi ya Kikorea.

M. M. Mulokozi na K. K. Kahigi (1979) wanaweka matumizi ya istiara na ishara katika kundi la sitiari pana. (9) Kwa ujumla sitiari ni namna moja ya kulinganisha kitu kimoja na kingine hali maana zake hufichika.

Tukiangalia methali za Kikorea zinazoibusha tamathali hii katika matumizi yake;

32. Fedha ni mwenye nguvu nyingi.

33. Uaminifu ndio hazina ya maisha.

34. Kanwa na tumbo ni maadui.

m.z. Binadamu hawezi kuishi bila chakula. Chakula hicho hakipatikani bure, bali huwa kinapatikana kwa kufanya kazi. Kufanya kazi mara kwa mara kunamshurutisha mtu kujiweka katika hali ya chini na hali hafifu, hali anaona uchungu moyoni mwake. Wafanyakazi wanapojilazimisha kuvumilia hali hii wao hutumia methali hii kwa stihizai.

35. Mgogoro kati ya mke na mume ni kukata maji kwa kisu.

m.z. Kitendo cha kujaribu kukata maji kwa kisu hakibakishi dalili wala sazo. Hata ingawa mke na mume wakigombana kuhusu swala fulani wanaafikiana kama tunavyoshuhudia katika kitendo cha kujaribu kukata maji kwa kisu.

2.3. Taswira za wanyama katika methali

Si ajabu 'kabinadamisha' wanyama au viumbe vinginevyo katika fasihi simulizi methali zikiwemo au kuwahayawanisha binadamu kwa ajili ya tabia zao maalum. Yaani watu huwachora wanyama au mimea wakiwa na tabia maalum, vivyo hivyo watu wanasawiriwa kama wanyama.

Maumbo ama tabia za wanyama au viumbe kwa ujumla hutumiwa kama ngenzo ya kuchora taswira hizo zinazolingana na hisia au sifa za binadamu.

Taswira hizo zinatiririka na kudhihirika hasa katika hadithi za mapokezi, na hadithi hizo zenye lengo la kuwafundisha watu maadili ya kijamii ni kichujwa murua cha fikira na imani za watu. Taswira hizo zinazotiririka katika hadithi za mapokezi hutangamana na taswira zinazoonekana katika methali.

Taswira hizo pengine zilitumiwa kuudhihaki utawala dhalimu wa kimwinyi, watawala wakatili wa karne hizo na maovu yaliyopachikwa na utawala giza wa kimwinyi.

Lipaswalo kuzingatiwa katika swala hili ni uhusiano ule kati ya mazingira na maisha ya binadamu. Kwa kuwa methali ni kama chakula kinachopikwa kwa kutumia mazingira na maisha yanayoathiriwa na mazingira hayo taswira za baadhi ya wanyama zinazosawiriwa katika jamii fulani hazionekani katika jamii nyingine.

Kwa mfano wazaliwa wa jangwani hutumia mazingira yanayozingira jangwa katika fasihi na tanzu nyinginezo za kiutamaduni. Dilevile hisia zinazohisika kuhusiana na mvua zitatofautiana kati ya nchi za baridi na za kitropiki. (10)

Katika methali za Gikuyu ni nadra sana kuziona methali zenye taswira za samaki (11), hali Waswahili wanatumia taswira za samaki

kama vile papa, ngisi, nguva na pweza. Tukiangalia taswira za papa katika fasihi simulizi kwa ujumla wanasawiriwa kuwa na uchoyo.

Hali kadhalika chui wa Bara Hindi anayejitokeza mara nyingi katika methali za Kikorea haonekani katika methali za Kiswahili kwa kuwa mnyama huyu haishi katika eneo la Afrika Mashariki. Lakini wanyama kama chui na simba ambao wanajitokeza sana katika methali za Kiswahili hawaonekani katika methali za Kikorea.

Isitoshe mazingira yanayowazunguka Wakorea katika maisha yao ni milima mikubwa na mirefu na bahari, kwa hivyo wana methali nyingi kuhusu milima na bahari. Wanyama wanaojitokeza mara nyingi katika methali za Kikorea ni chui wa Bara Hindi, mbwa, paka, kunguru, kuku, punda, nguruwe, farasi, ndege, ng'ombe, panya, sungura na joka. (12)

Kwa upande wa methali za Kiswahili wanyama wanaojitokeza mara nyingi ni kuku, ndege, ng'ombe, paka, nyoka, punda, samaki, simba, ndovu na jogoo.

Hapa tutaangalia taswira za baadhi ya wanyama kwa mbinu ya ulinganishi tukitoe methali kadha wa kadha ambazo zinaibusha taswira hizo.

1. Chui wa Bara Hindi (Tiger)

Mnyama huyu anajitokeza mara nyingi katika methali za Kikorea, ilhali haonekani katika methali za Kiswahili kwa kuwa mnyama huyu

haishi katika Bara la Afrika. Kama tulivyotangulia kuiangalia taswira ya chui wa Bara Hindi inayodhihirika katika methali za Kikorea sifa zake huhusiana na ujasiri, uhodari na ukali.

Kuhusiana na taswira na sifa za chui wa Bara Hindi

F.J. Seligson (1989) anasema;

Katika hadithi za mapokezi zilizorithishwa kizazi kwa kizazi, chui wa Bara Hindi mara kwa mara anasimuliwa kama kitu kikubwa na hafifu cha kuchezea kwa tafrija ya sungura. Kwa upande mwingine chui wa Bara Hindi ni kiumbe mwenye busara na ukarimu, mtumishi wa Mungu wa mlima (the mountain God) ambaye anajigeuza kama chui wa Bara Hindi mweupe wakati ambapo anakagua milki yake. Kwa hakika sifa za chui wa Bara Hindi zimeingia sana ndani ya roho za Wakorea kwa kuwepo kwake kwa kutisha kulikoaminiwa kuwa mnyama mlinzi wa taifa (13). (tafsiri yetu)

Kama picha halisi ya uhodari, ujasiri na wema amechukua nafasi muhimu katika roho za Wakorea. Yafaa kuangalia baadhi ya methali za Kikorea zenye taswira na chui wa Bara Hindi.

36. Ukisema chui wa Bara Hindi atakuja.

m.z. Methali hii hutumiwa kututahadharisha tusimsengenge mtu, hali hayuko katika mazungumzo

yetu. Mtu akijitokeza wakati anaposengenywa na watu hutumiwa methali hii. Katika jamii ya Wakorea chui wa Bara Hindi alikuwa mnyama wa kuwatisha na kuwaogofya watu, hali ibilisi au shetani alikuwa mwenye kuwaogofya na kuwatisha watu katika jamii ya Waingereza ambapo dini ya Kikristo ilikuwa msingi katika maisha yao. Methali ya Kiingereza Speak of devil (Ongelea ibilisi) inafanana na methali hii katika matumizi na maana yake. Dennis Dunham (1986) anaeleza kwamba methali hii ya Kiingereza ilianza kutumiwa kuanzia karne za katikati (mediaeval times). Wakati huo Waingereza walikuwa na imani mbalimbali za ushirikina na mojawapo ya imani hizo ilikuwa ya kwamba njia nzuri ya kumzuia shetani au ibilisi asiingie nyumbani ilikuwa kutosema kuhusu shetani. (14)

37. Sungura hujifanya kama mkubwa katika mahali ambapo hayupo chui wa Bara Hindi.

m.z. Chui wa Bara Hindi alikuwa mfalme wa wanyama wote katika hadithi za mapokezi. Sungura ni mnyama mdogo, lakini anasawiriwa kama mnyama mwenye busara inayoambatana na ujanja. Chui wa Bara Hindi akiondoka, sungura hujifanya kama mkubwa au mwalimu bila kuogopa. Katika methali hii sungura huashiria mtu mwenye busara na ujanja na chui wa Bara Hindi ni mfano wa mtu mwenye nguvu na

mamlaka ya kutawala. Methali ya Kiswahili ifananayo na methali hii katika matumizi na maana yake ni Paka akiondoka panya hutawala.

38. Usipoingia ndani ya pango la chui wa Bara Hindi huwezi kumwinda hata mtoto wake.

m.z. Kuingia ndani ya pango la chui wa Bara Hindi ni kazi ngumu inayohitaji ujasiri na uhodari na kumwinda mnyama huyo au hata mtoto wake ni zawadi au pato analopewa mtu anayethubutu kukabili hatari na uchungu pasi na woga wala kusitasita.

II. Simba

Inaelekea kwamba taswira na sifa za simba zinazohisika katika methali za Kiswahili zalingana kwa kiasi kikubwa na za chui wa Bara Hindi katika methali za Kikorea. Mnyama huyu haonekani katika methali za Kiswahili. Katika mashairi ya Muyaka mnyama huyu anasawiriwa kama shujaa, mtu hodari na mwanamume mwenye ujasiri.(15) Kwa ujumla simba husawiriwa kuwa mnyama wa ujasiri, uhodari na nguvu za kiume.

- . Inzi hatui juu ya damu ya simba.
- . Angurumapo simba, mcheza nani?
- . Usicheze na simba, ukamtia mkono kinywani.
- . Usiombe kukutana na simba.

III. Nguruwe

Aghalabu nguruwe husawazishwa na dhana zisizo nzuri kama vile uchafu, uduni na uhafifu katika methali za Kikorea na za Kiswahili. Katika jamii ya Wakorea kila mara wanapoanzisha shughuli maalum au kufungua ofisi kirasmi wanaweka kichwa cha nguruwe madhabahuni kama sadaka. Zaidi ya taswira zake kama vile uchafu, uhafifu na uduni pia anawakilisha sifa mbaya za ukosefu wa maadili na uchoyo.

Kutofautiana na taswira hizi nguruwe ni alama ya mafanikio, ustawi na utajiri. Dilevile ndoto ya nguruwe kabla ya wanawake kutunga mimba huashiria kuzaliwa kwa mtoto wa kiume. (16)

Tukiangalia taswira za mnyama huyu katika methali za Kikorea na za Kiswahili;

39. Nguruwe hupenda maji machafu.

m.z. Methali hii inatumiwa kudokeza kwamba mchafu hushirikiana na mchafu mwenzake.

40. Kufuli ya shaba kwa zizi la nguruwe.

m.z. Shaba ni aina mojawapo ya madini ambayo hung'ara na zizi la nguruwe ni pachafu. Uitu hivi viwili havilingani. Mfano mmoja wa matumizi ya methali hii ni mwanamke anayejaribu kujirembesha na kujipamba kwa nguo ghali na mapambo mengineyo, hali ana umbo na sura ya kuchukiza.

41. Nguruwe anayelala chali humshutumu mwenzake
anayekalia matako.

m.z. Katika maisha ya binadamu mwenye kuzidi kuwa
na dosari na makosa huwalaumu wenzake ambao
hawana dosari na makosa mengi.

42. Mwenye kuzaliwa mwaka wa nguruwe
hutajirika. (17)

Methali zinazofuata ni methali ambazo zinaonyesha taswira za
nguruwe katika methali za Kiswahili;

- . Nguruwe hawezi kuacha vihama.
- . Ukitaka kula nguruwe chagua aliyenona.

m.z. Waislamu hawaruhusiwi kula nyama ya
nguruwe. Waswahili wameathiriwa sana na dini
ya Kiislamu.

III. Punda

Taswira za punda zinazoibuka katika methali za Kikorea na za
Kiswahili huwa ni ukaidi, ushupavu, utovu wa shukrani na ukosefu wa
adabu. Taswira hizi hutokana na hadithi simulizi au tabia za mnyama
hugo.

43. Punda arembesha sikio lake.

m.z. Masikio ya punda huwa hayapendezi macho ya watu. Arembesha masikio yake au la ni mamoja. Mara nyingi watu wakijaribu kurembesha pasipostahili kutiliwa urembo, hapo ndipo panakuwa panapoyachukiza macho ya watu.

44. Punda mpumbavu asiye na adabu humdharau hababu yake muungwana.

m.z. Wakati mtu hafifu akosaye adabu njema anapomsumbua muungwana asifikaye kwa wema na adabu nzuri ndipo methali hii inapotumiwa.

- . Msi nadhari ni punda, msi kujua endako.
- . Ahsante ya punda ni mateke.
- . Fadhili za punda ni mashuzi; na msihadhari ni ng'ombe.
- . Punda hana fadhili.
- . Punda haendi bila mchapo.
- . Punda haendi ila kwa kigongo.

Mbali na taswira hizo za ukaidi, ushupavu, utovu wa fadhili na shukrani kama zinavyosawiriwa katika methali hizi, mnyama huyu ni picha halisi ya wanaonyonywa, wanaotawaliwa na wanaodhulumiwa katika jamii yenye matabaka. Methali inayofuata ni dhihirisho la hali ya unyonge katika taswira ya punda.

- . Hufanya kazi punda, matai humpenda.

D. Sungura

Tukiangalia taswira mbalimbali za mnyama huyu katika hadithi za mapokezi na methali mara nyingi anasawiriwa kama mjanja, mwerevu na mwenye hila. Ijapokuwa mnyama huyu hajitokezi mara kwa mara katika methali za Kiswahili sifa zake ni hila na ujanja;

. Duma hukamata, sungura hupata.

. Hila za sungura, kulia kwa vyura.

Taswira hii pia inabainika katika methali za Kikorea. Kama tuliyoangalia katika taswira ya chui wa Bara Hindi;

45. Sungura hujifanya kama mkubwa katika mahali ambapo hayupo chui wa Bara Hindi.

SURA YA PILI

Tanbihi

1. Clark, Virginia P., Eschholz, Paul A. and Rosa, Alfred F. (1981),

Language Introductory Readings Third

Edition New York; St. Martins Press, Inc., Uk. 46.

Kuna mifano mingi ya kueleza uhusiano uliopo kati ya lugha na mazingira. Washona wanaoishi nchini Zimbabwe wanayo maneno matatu muhimu tu yahusuyo rangi; *cipsuka* (rangi ya machungwa, rangi

yahusuyo rangi; *cipsuka* (rangi ya machungwa, rangi nyekundu, rangi ya zambarau bivu na blu); *citema* (blu na rangi ya majani); na *cicena* (rangi ya majani na ya manjano). Uk. 46.

2. Lee, Kyu Tae (1987), Taaluma ya Korea ya Machozi,

Seoul; Kampuni ya Uchapishaji ya Kirinwon. Uk. 261.

Katika kitabu hiki chenye kuandikwa kwa mtindo wa kiinsha mwandishi anatuchorea taswira mbalimbali zinazohusika na matukio ya kihistoria, mila, desturi, maadili ya kijamii, maisha, mambo ya kijadi na kadhalika.

3. Hastings, James (1921), Encyclopaedia of Religion and Ethics Volume XII. Edinburgh; T.&T. Clark. Uk.

396.

4. Ha. T.B. and Mintz, G.K.(1972), Samkuk Yusa (The History of the Three Kingdoms) Tafsiri ya Kitabu cha Ilyon, Seoul; Yonsei University Press.

Kitabu hiki kinachohadithia kuanzishwa kwa taifa la kwanza kwenye Rasi ya Korea kiliandikwa na mtawa wa kibudha aliyemitwa Ilyon mnamo mwaka wa 1289. Wataalamu wanadokeza kwamba hurafa ya *Tangun* inahusiana na *Wabainu* wanaoishi katika sehemu za

Kaskazini nchini Japan kwa sababu ya ibada yao ya dubu. Hurafa hii ya *Tangun* huchukua nafasi muhimu sana katika uchunguzi wa historia na imani za Wakorea. Ingetufaa kuangalia hadithi nzima ya hurafa hiyo inayofuata;

Hapo zamani mwana wa mfalme wa Peponi alitamani kuteremka ulimwenguni. Siku moja yule mwana wa mfalme alimwuliza babake "Ni nani anaishi kule?" akielekeza kidole chake upande wa ulimwengu. "Ujumbe wengi kama vile wanyama, ndege na samaki wanaishi kule", babake akamjibu. "Ujumbe kunaishi miti mingi, maua na ujumbe wa ajabu wanaoitwa watu". Mwana wa mfalme aliyeitwa *Hwan-ung* aliposikia hivyo, tumaini lake la kutembelea ulimwenguni lilizidi kuliko hapo awali. Yule mfalme wa Peponi ambaye alikuwa ameshatambua matakwa ya mwanake aliamua kumtafutia mahali murua zaidi.

Aliiangalia mifululizo mitatu ya milima mikubwa kwa uangalifu na makini na hatimaye akauchagua *Mlima Taebaek* ulioko kaskazini mwa Korea kama pazuri zaidi penye manufaa kwa mwanake. Hivyo basi alimwita mwanake kumwambia habari njema. Akamwambia mwanake "Nitakuruhusu uende ulimwenguni kujenga taifa jipya. Ni wajibu wako

kuwafundisha wananchi wa taifa lako jinsi ya kupendana wakati wa shida. Nitawatuma watumishi elfu tatu watiifu kushirikiana nawe", akaongeza yule mfalme wa Peponi.

Kwa ajili hii, mwana wa mfalme wa Peponi alikuja hapa ulimwenguni. Kwa mara yake ya kwanza alijitokeza chini ya msandali. Hapo alianzisha kijiji chake na kuita Mji wa Mungu. Akawa *Chonwang* lenye maana ya mfalme wa Peponi. *Chonwang* alisifika kwa utawala mwema na aliwafundisha wananchi wake kazi na stadi mbalimbali kama vile kilimo, utabibu, useremala, ushonaji na uvuvi kusudi wote wanufaike kwa stadi na kazi zao. Aliimarisha kanuni zenye maadili na sheria zifaazo na kuwahimiza wananchi wake waziheshimu. Ujumbe wote wakiwemo binadamu na hata wanyama vilevile walipata kumheshimu kama kiongozi wao. Kuliishi dubu mmoja na chui wa Bara Hindi, ambao walitumai sana kuwa binadamu katika kijiji hicho. Walitaka kusimama kwa miguu miwili kama wanavyoweza binadamu. Kwa hivyo walimtembelea Mfalme *Hwan-ung* wakamwomba awawezeshe kuwa binadamu. "Tafadhali tusaidie tuwe binadamu tukaishi maisha murua" dubu na chui wa Bara Hindi wakamwomba Mfalme *Hwan-ung*. "Yawezekana" akajibu mfalme, "lakini, itakuwa ni

uigumu mno kutekeleza kazi hiyo, kwa sababu hiyo lazima muumilie machungu ya kazi hiyo bila kulalamika". "Hata kama iwe kazi ngumu inayohitaji ustahamilivu usiokuwa na kifani, tutavumilia tu", yule chui wa Bara Hindi na dubu walimwahidi. Mfalme yule aliwahurumia na kukubali kuwasaidia wawe wanadamu. Mfalme alimpatia kila mmoja wao kichala kimoja cha pakanga na pauni mia moja na sitini za vitunguu saumu. "Endapo mtakula chakula hichi kitakatifu na hamtaangalia mwanga wala nuru ya jua kwa siku mia moja mfululizo, mtakuwa wanadamu", akasema mfalme. Dubu na chui wa Bara Hindi walikichukua chakula hicho na kuingia ndani ya pango kubwa. Lakini walipoanza kula chakula hicho walirindima kwa ukali na uchungu wa chakula hicho. Vitunguu saumu vilikuwa vikali mno na viliwasha midomo yao na pakanga ilikuwa chungu sana kwao. Wakagundua kwamba kazi waliyopewa siyo rahisi kutekeleza, bali ni ngumu kupita kiasi.

Baada ya siku chache yule chui wa Bara Hindi alianza kunung'unika. Alikuwa na uhakika wa kwamba kitunguu saumu chake kilikishinda cha dubu katika ukali wake wa kuwasha mdomo. "Ninakichukia chakula hiki ambacho tunashurutishwa kukila. Nimekuwa na hamu ya kuangalia mwanga murua wa jua na hewa safi nje ya pengo hili lenye giza tororo",

aliendelea kulalamika. "Jikumbushe tuliambiwa kwamba tuwe wastahamiliu ikiwa tunatarajia kufaulu", dubu yule alimfahamisha chui wa Bara Hindi. Hata hivyo, chui wa Bara Hindi mwenye harara aliendelea kunung'unikia kutobahatika kwake. "Kama tungetoka nje kwa dakika chache na kupumua hewa safi na kurudi, ingekuwa kama ndoto", akapendekeza chui wa Bara Hindi. Walakini, msimamo wa dubu ulikuwa imara bila kushawishiwa na chui wa Bara Hindi na alikataa kutoka nje. "La hasha! tuliambiwa kwamba lazima tukae hapa kwa siku mia moja mfulilizo", dubu akajibu. Alijaribu kumtuliza chui wa Bara Hindi, akimwambia ajikaze na avumilie machungu na matatizo yote ili awe binadamu. Baada ya majuma machache yule chui wa Bara Hindi hatimaye alipiga yowe, "Siwezi kuvumilia zaidi. Ukali wa chakula na giza totoro zinapita ustahamiliu wangu". Yule dubu alijaribu mara moja zaidi kumhakikishia chui wa Bara Hindi kwamba ni lazima avumilie kidogo zaidi ili kutimiza matumaini yake ya kuishi kama binadamu. "Kama unazingatia maisha yako ya siku za usoni ambapo utaishi kwa upeo wa furaha kama binadamu na kusimama wima kwa miguu miwili, siku mia moja si muda mrefu kama unavyofikiri", akasisitiza dubu. "Siwezi kuvumilia hali hafifu!", chui wa Bara Hindi akapiga yowe gizani. "Niwe binadamu nisiwe binadamu, mimi sijali. Nitoke

nje ya pango hili musimopita hewa na nile chakula kitamu kujiburudisha". Mara alipomaliza kunena hivyo, akatoroka kutoka pango lenye giza totoro kuelekea penye mwanga wa jua. Alikopesakopesa macho akiangalia mwanga wa jua linalochomozea wakati wa asubuhi. Kila kitu kilionekana kizuri na kinachopendeza. Sauti ya kijito ikasikika kwa masikio yake na akeanda huko kunywa maji safi yaburudishayo. "Kwa hakika ulimwengu huu umeumbika vizuri na mandhari ya kushangaza na ulimwengu huu unatupatia nyemi na raha za kweli. Kwa nini nimejisumbua na kujikalifisha kukaa na yule dubu mjinga pangoni ambamo mna giza tupu tu", akajiuliza yule chui wa Bara Hindi. Hakuwa na nia ya kurudi pangoni tena. Chui wa Bara Hindi hakuweza kuwa binadamu, bali alibakia mnyama huyo huyo kwa maisha yake yaliyosalia, madhali alishindwa kukamilisha masharti ya Mfalme *Hwan-ung*. Lakini, dubu huyo aliendelea kukaa ndani ya pango lenye giza na kutekeleza masharti ya Mfalme *Hwan-ung*. Hatimaye kiroja kikatokea.

Manyoya ya dubu yakatoweka na umbo lake likabadilika kuwa mwanamke mrembo sana. Baada ya siku mia moja kupita alitoka nje ya pango na kuketi chini ya msandali uliokuwa na karibu na mlango wa pango hilo. Halafu aliomba dua abarikiwe

kutungwa mimba. Mfalme *Hwan-ung* alipomwonamwanamke yule akavutiwa naye mno kwa urembo wake. Wakaoana na kupata mtoto wa kiume amabaye aliitwa *Tangun Wanggom*, yaani Mfalme wa Msandali. *Tangun* alikua akawa shujaa hodari mwenye akili. Alikuwa kwenye kisiwa cha *Kanghwa* na kujenga madhabahu ya ibada katika kileleta cha kisiwa hicho. Aliwaahidi wazazi wake kujenga taifa jipya. Aliondoka kwake kuelekea upande wa kusini. Akafika kwenye ukingo wa *Mta Taedong*. Katika maeneo yaliyoko ukingoni mwa *Mta Taedong*, akaanzisha mji mkuu ulioitwa *P'yongyang*. *Tangun* aliuita ufalme wake *Choson* na ulimaanisha Nchi ya asubuhi Shwari (Land of the Morning Calm). Hivi ndivyo taifa la Kikorea lilivyoanzishwa na *Tangun* anaheshimiwa kama mwanzilishi wa taifa na mfalme wa kwanza miongoni mwa Wakorea. Mke wake *Tangun* aliwazaa watoto watatu wa kiume, ambao walirudi kisiwani *Kanghwa* ili wamwabudu Mungu katika madhabahu iliyojengwa na baba yao. Ulevile wakajenga ngoma imara tena ndefu kwa siku moja tu. Ufalme ulioanzishwa na Mfalme wa Msandali ulidumu kustawi kwa muda mrefu upatao miaka elfu mbili mfululizo.

5. Seligson, Fred Jeremy (1986) Some Thoughts on *Tangun*, An article in the Journal of Hankuk University of

Foreign Studies Vol. 19, Seoul: Hankuk University
of Foreign Studies Press. Uk. 498.

6. Mbaabu, Ireri (1985), Utamaduni wa Waswahili, Nairobi:
Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd. Uk
42.

7. Korea, Its Land, People and Culture of all Ages (1960),
Seoul: Hakwon-sa, Ltd. Uk. 37.

8. Abdulaziz, M.H. (1979), Muyaka 19th Century Swahili
Popular Poetry, Nairobi: Kenya Literature
Bureau. Uk. 63.

Mashairi ya Muyaka yanalinganishwa kama bahari ya jazanda, fumbo, istiara, sitiari na ishara. Mishororo mingi katika mashairi ya Muyaka inatumiwa katika methali za Kiswahili kwa upana. Hatuna uhakika kwamba Muyaka alizitumia methali hizo katika mashairi yake au mashairi yenyewe yakawapendeza Waswahili katika umahiri wake wa matumizi ya lugha mpaka baadhi ya mishororo ikatumiwa kama methali. Ingawa kuna methali nyingi za Kiswahili zinazoonekana katika mashairi ya Muyaka, tunatoa baadhi ya mifano;

. Njia mbili zaumiza.

- . Kuvua numbi si kazi, kuu ni magawioni.
- . Majuto huja kinyume.
- . Msema pweke hakosi, haijui aliye.
- . Kifo kikimbizwa funza chawekwa mahali gani.
- . Mwenda mbizi nti kavu yuatunua usowe.
- . Hindi ndiko kwenyi nguo, na waendao tupu wako.

9. Mulokozi, M.M. na Kahigi, K.K. (1979), **Kunga za Ushairi na Diwani Yetu**, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House. Uk. 39.

10. Kwa mfano wa Thiong'o, Ngugi (1981) anatueleza swala hili kutokana na tajiriba yake ya kibinafsi. **Writers in Politics**, Nairobi: Heinemann Educational Books Ltd. Uk 3-4.

11. Angalia methali za Gikuyu katika Kitabu cha **Gikuyu za Proverbs** (1969), London: Mcmillan and Co. Ltd.

12. Tumetumia neno 'joka' kumaanisha 'dragon' kwa lugha ya Kiingereza. Mnyama huyu hayuko katika ulimwengu halisi, bali anawazika katika mawazo ya binadamu. Mnyama huyu anaaminiwa kufanana na nyoka mkubwa katika umbo lake. Ana magamba themanini na moja mgongoni, sura ya kutisha, pembe, masikio,

sharubu na miguu minne. Dilevile ana uwezo wa kuzama majini na kuruka mbinguni. Anaweza kutengeneza mawingu na kunyesha mvua. Kufuatana na hurafa mbalimbali za nchi za Mashariki ya Mbali mnyama huyu a nagesawiriwa katika hadithi kama ndege wa 'Phoenix' ni alama ya ufalme na utukufu. Kwa sababu hii sura ya mfalme huitwa sura ya mnyama huyu (*Yongari*), vivyo hivyo nguo ya mfalme kama nguo ya mnyama huyu (*Yongpa*), kitanda cha mfalme kama kitanda cha mnyama huyu (*Yongsang*) na kadhalika.

13. Seligson, Fred Jeremy (1989), **Oriental Birth Dreams**, New Jersey: Hollym International Corp. Uk. 143.
14. Dunham, Dennis (1986), **Kumfundisha Samaki Jinsi ya Kuogelea**, Seoul: The Si-sa-yong-o-sa Publishers, Inc. Uk. 232.
15. Tazama ubeti wa IU katika shairi la **K'ongowa ja mvumo na ubeti wa kwanza katika shairi la Itakapo kukutana** Abdulaziz, M. H. (1979), **Muyaka 19th Century Swahili Popular Poetry**, Nairobi: Kenya Literature Bureau. Uk. 146 na 156.

16. Seligson, Fred Jeremy (1989), Oriental Birth Dreams, New Jersey: Hollym International Corp. Uk. 153.

Anafafanua asilimia sabini na sita ya wanawake wanaoota ndoto ya nguruwe kabla hawajitunga mimba huwa wanajifungua mtoto wa kiume.

17. Ili kuelewa maana ya methali hii inatubidi kujua ushirikina

wa Wakorea. Wakorea wanatumia mbinu maalum katika kuhesabu miaka. Kwa mfano mwaka huu wa 1992 ni mwaka wa nyani kufuatana na mpangilio mahususi unaofuata;

- 1) panya 2) ng'ombe 3) chui wa Bara Hindi
- 4) sungura 5) joka la kihadithi (dragon) 6) nyoka
- 7) farasi 8) kondoo 9) nyani 10) kuku 11) mbwa
- 12) ngurwe.

Iko hadithi ya zamani kuhusu wanyama hao kumi na wawili. Hapo zamani za kale Mungu aliwaambia wanyama wote wa dunia. "Kesho ni sikukuu ya mwaka mpya. Mtanitembelea kunisalimia kama mliyofanya kwa desturi katika sikukuu ya mwaka mpya ya miaka mingine iliyotangulia. Lakini mnashauriwa kunitembelea kwa haraka na upesi zaidi kuliko sikukuu ya mwaka mpya ya miaka iliyopita. Mnyama atakayewasili mapema zaidi kuwashinda wanyama wengineo atatuzwa zawadi." Ng'ombe aliondoka mapema wanapolala wanyama wengine,

madhali alijua kwamba yeye si hodari katika mashindano ya mbio. Wakati huo huo panya alimwona n'gombe akiondoka na akakimbilia na kupanda juu ya mgongo wa ng'ombe. Walipofika mbele ya mlango wa Kasri ya Mungu panya akateremka kutoka kwa mgongo wa ng'ombe na kuingia ndani ya mlango kabla ya ng'ombe kuingia. Kwa hivyo panya alikuwa wa kwanza katika mashindano hayo ya mbio. Sungura alifika amechelewa kwa kuwa alilala fofoto.

Wanyama hao kumi na wawili waliwasili mmoja baada ya mwingine. Mungu aliwapatia wanyama hao wote majina ya mwaka kufuatana na utaratibu wa mashindano ya mbio.

Mpaka siku hizi Wakorea wanaulizana "Ddiyako ni nini?" (yaani, ulizaliwa katika mwaka wa mnyama gani?) badala ya kuuliza "Una umri gani?" (yaani, ulizaliwa lini?). Wakorea wanapochagua bibi na bwana arusi wanashikilia imani hii ya ushirikina. Wanaamini kwamba uhusiano baina ya nyani na mbwa ni mbaya, hivyo basi mtu mwenye kuzaliwa mwaka wa nyani akifunga ndoa na mzaliwa wa mwaka wa mbwa watagombana na kukosana kila wakati. Hata katika methali kunadhihirika uhusiano huo mbaya kati ya nyani na mbwa.

46. Uhusiano baina ya mbwa na nyani.

Mutiso, Kineene (1987), Utamaduni wa Wakorea, Seoul: Shirika la
Uchapishaji la Chuo Kikuu cha Masomo ya Kigeni cha Hankuk. Uk. 82-83.

SURA YA TATU

3.0. Utangulizi

Katika sura hii tutajishughulisha na maudhui mbalimbali yanayodhihirika katika methali za Kikorea na za Kiswahili kwa njia ya ulinganishi. Swala linalotiliwa maanani na uzito zaidi katika sura hii ni ufanano na tofauti katika methali za jamii hizi mbili. Sura hii imegawanyika katika sehemu tatu.

Ya kwanza itakuwa na maelezo kuhusu mbinu inayotumiwa kuzipanga methali. Katika sehemu hii tutaeleza mbinu kadha wa kadha katika upangaji wa methali na kufafanua vifupisho na alama zinazotumiwa.

Ya pili ni sehemu ambapo tutaangalia maswala kadha wa kadha kuhusiana na uainishaji wa methali kimaudhui. Tutapitia mbinu za C.L. Sibusiso Nyembezi (1963) na Chung, Chong Hwa (1991) ambazo zinaingiliwa na ubinafsi wao katika kutenga makundi ya maudhui mbalimbali.

Ya tatu ni uti wa mgongo katika kazi yetu. Methali za Kikorea zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili zitalinganishwa na za Kiswahili. Ili kutosheleza lengo letu au kufahamu ujumbe zaidi tutaangalia methali za jamii zinginezo zenye kufanana kimaudhui na methali za Kikorea na za Kiswahili.

3.1. Upangaji wa methali

I. Upangaji wa methali

Kwa kuwa lililo muhimu zaidi katika kazi yetu ni falsafa na mawazo ya watu katika fani ya methali hatutatilia mkazo mtindo wala fani katika methali.

Tutatafsiri methali za Kikorea kwa lugha ya Kiswahili na kuziweka methali zifananazo kimaudhui pamoja. Katika kuitafsiri methali moja ya Kikorea methali hiyo inaweza kutafsiriwa kwa namna mbalimbali na tutaonyesha tafsiri zote. Dilevile hatutaonyesha kwa hati za Kikorea katika tafsiri.

Kwa methali zenye kuhitajika kuongezwa maelezo maalum ili kuelewa maana yake tutaongeza maelezo. Kwa mfano baadhi ya methali hazifahamiki bila kuelewa maneno yanayotumiwa katika methali hizo. Maneno hayo, kwa kawaida, yanahusu majina ya kijiografia, matukio ya kihistoria, desturi au mila za kijamii, mambo ya kidini na mengineyo. Tukiangalia mifano inayoonyesha jambo hili;

47. Ni mjumbe aliyepelekwa mjini *Hambung*.

m.z. Wakati wa enzi ya ufalme wa *Yi Taejo* aliyekuwa mwanzilishi wa ufalme wa *Yi* alikosana na mwana wake *Taejong* ambaye alikuwa mfalme wa pili katika ufalme huo. Kwa sababu ya kukosana na mwanake *Taejong* alikwenda *Hambung* na hakurudi kwenye

kasri. Hivyo basi *Taejong* alihangaika moyoni mwake. Akamtuma mjumbe ili kutuliza hasira za babake. Lakini kila mara mjumbe alipotumwa huko *Hambung* aliuawa na hakuweza kurudi. Kwa sababu ya tukio hilo la kihistoria mtu yeyote aliyetumwa kwa shughuli fulani asiporudi hata baada ya muda mrefu, methali hii hutumiwa. (1) Lakini asiyejua tukio hilo la kihistoria hataweza kuelewa maana yake na matumizi yake.

48. Mtawa wa kibudha hawezi kukata nywele zake.

m.z. Mtu yeyote anayetaka kuwa mtawa wa Kibudha anyolewe nywele zake kama alama ya kujitenga na mambo ya dunia. Mtu huyo hawezi kujinyoa mwenyewe, bali hunyolewa na mwenzake.

49. Aliyepigwa kofi katika *Chongno* hutazama kitongotongo katika *Mta Han*.

m.z. Mtu anayekasirika katika mahali fulani akitoa ghadhabu hizo mahali pengine methali hii hutumiwa kumpuuza. Wataalamu wa elimunafsi wanadai kwamba kitendo cha namna hii huitwa 'Displaced Aggression'. (2) *Chongno* ni sehemu moja iliyoko katika mji wa Seoul na *Mta Han* unapita mjini Seoul.

Kama tulivyotoa baadhi ya methali zinazohitaji maelezo maalam tutajaribu kueleza mambo mbalimbali ambayo ni ufumbuzi wa maana

zake. Lakini methali zile zinazofahamika kwa urahisi bila kuwa na maelezo maalum hazitaongezwa maelezo hayo.

Methali za Kikorea hubainika na kugawanyika kati ya methali zenye asili ya Kikorea na methali zenye asili ya Kichina. Methali hizo zenye asili ya Kichina ambazo huwa zinasisitiza mafundisho ya kimaadili zimetafsiriwa kwa lugha ya Kikorea na kushika mizizi katika utamaduni wa Wakorea. Nchi ya China na Korea zimeathiriana kiutamaduni, kihistoria na kisiasa. Taathira hizo zimetawanyika na kunyungizika kwenye nyanja mbalimbali za maisha ya Wakorea. Utamaduni wa Wachina umerutubisha utamaduni wa Wakorea. Lakini Wakorea walipopokea utamaduni wa Wachina walijitahidi kuyachuja mambo kadha wa kadha yanayoweza kuleta kasumba ya ukoloni wa kiutamaduni.

Katika kazi yetu tutahakiki methali zenye asili ya Kichina ambazo zikawa za Kikorea kindakindaki. Hakuna utamaduni usohadhari: usioingiliana na tamaduni nyingine.

Tutaweka nambari katika kila methali ya Kikorea. Methali zinazofanana zimewekwa pamoja ziwe kundi moja. Vilevile methali zinazoandikwa kwa lahaja zitapangwa pamoja na methali zinginezo.

II. Ufafanuzi wa vifupisho na alama

Tutatumia baadhi ya uifupisho na alama katika kazi yetu kwa madhumuni ya kurahisisha kuzifahamu methali. Ufafanuzi wa uifupisho na alama hizo ni;

1) *taf.* = tafsiri

Tutajaribu kuzilinganisha methali za jamii ambazo zinafanana sana kimaudhui na kuongesha asili yake katika mbano. Iwapo methali hizo zimeandikwa kwa hati za Kirumi tutaziweka methali hizo zengewe na halafu tutaongeza tafsiri yake.

2) *m.z.* = maelezo

3) *ta.z.* = tazama

Kuna methali nyingi zilizo sawa katika maudhui na ujumbe wake, lakini ambazo zina maumbo tofauti na maneno mengine. Tutaweka methali hizo zote pamoja.

4) * = alama ya maelezo ya maneno yanayotatiza.

5) () = mbano duara hutumika kuongesha asili ya methali.

3.2. Uainishaji wa methali kimaudhui.

Kama tuli vyotangulia kuangalia uzuri na udhaifu unaojitokeza katika mpangilio wa kiabjadi hakuna mbinu maalum inayokamilika na kutosheleza kikamilifu matilaba ya anuiaye kuchambua methali.

Hata hivyo, linalotufanya kuchagua mbinu ya kuziainisha methali kimaudhui ni kwamba tunaazimia kuchakura jinsi watu wanavyoyasawiri mambo au matukio mbalimbali yanayowazingira katika methali.

Isitoshe, tunakusudia kulinganisha kule kufanana na kutofautiana kwa fikira au mawazo yanayojitokeza katika methali. Yatupasa tupekue ni nini kinacholeta mitazamo itofautianayo kuhusu swala moja na tujadili iwapo watu wana mitazamo ifananayo kukabiliana na swala maalum inaposadifu kufanana au kulikuwa na maingiliano na mawasiliano ambayo yangeleta kule kulingana.

Ditabu vitatu muhimu vyenye kutunufaisha zaidi katika uainishaji wa methali kimaudhui ni vifuatayo; C.L. Sibusiso Nyembezi (1963) ametenga makundi kumi makubwa kulingana na umuhimu wa kiujumla na kuweka vijikundi vidogo chini ya makundi makubwa. Makundi hayo makubwa yana dhana kuu au ya ujumla ambayo inachukua dhana dogo zilizomo ndani ya vijikundi.

Tuangalie jinsi alivyoainisha Nyembezi (1963);

1. Utu

a) Ukarimu

- b) Tabia mbaya
- c) Fahari
- d) Utovu wa shukrani
- e) Ukaidi
- f) Utovu wa utu mwema na maadili murua
- g) Mengineyo yanayohusika na utu

2. Uaminifu na utovu wa uaminifu

- a) Udanganyifu
- b) Hila
- c) Utovu wa uaminifu

3. Urafiki na uhasama

- a) Utitisho
- b) Kisasi
- c) Utovu wa huruma
- d) Uadui
- e) Urafiki
- f) Uhasama
- g) Mengineyo yanayohusika na urafiki na uhasama

4. Bahati njema na bahati mbaya

- a) Bahati njema
- b) Bahati mbaya
- c) Taabu
- d) Kazi bure

- d) Kutofaulu
- f) Kukata tamaa
- g) Tashwishi
- h) Kutia moyo

5. Ujasiri na woga

6. Mambo ya nyumbani

- a) Ndoa
- b) Urithi
- c) Uendelezaji wa nyumba
- d) Uzawa
- e) Wazazi na watoto
- f) Mizimu
- g) Mazungumzo
- h) Mwazimo
- i) Mengineyo yanayohusu mambo ya nyumbani

7. Mapito ya wakati

- a) Uzee
- b) Kifo

8. Busara na ujinga

9. Tahadhari

- a) Malezi ya watoto
- b) Hatari

- c) Kufanya mambo mwenyewe
- d) Kutafuta mashauri
- e) Madhara ya vitu vidogo
- f) Kufanya mambo bila kuajizi
- g) Huruma kwa wengine
- h) Shukrani
- i) Utondoti
- j) Uvivu na jitihada
- k) Mengineyo yanayoihusu tahadhari

10) Mengineyo yasiyotengwa chini ya makundi tisa ya juu (3)

Chung, Chong Hwa (1991) ameyagawanya makundi kumi na manne na kuongeza vijikundi kadha wa kadha chini ya makundi makubwa.

Uainishaji wake watofautiana na wa C.L. Sibusiso Nyembezi kwa kiasi kikubwa. Ili kupata mwangaza kuhusu lisababishalo tofauti zile katika mambo yanayotiliwa msisitizo na uzito, inatufaa kuyazingatia maoni yake Chung (1991) kama yafuatavyo hivi;

Kuna tofauti katika dhana ya methali baina ya jamii ya Wakorea na ya Waingereza. Methali za Kikorea ni kiini cha utamaduni wa umma, ilihali methali za Kiingereza ni utamaduni wa tabaka la wastaarabu na wenye elimu kama inavyodhihirika katika methali hii Wenye busara huzitunga methali na

juha huzirudia methali hizo. Methali za Kikorea huwa zimetumiwa kudhihaki utawala mpotevu wenye giza ambao ulikuwa mbegu za njaa na udhalimu. Ulevile ukoo hutiliwa uzito zaidi kuliko mtu binafsi katika methali za Kikorea.

Kutofautiana na sifa zinazopatikana katika methali za Kikorea, methali zenye kutilia mkazo na umuhimu kwa utulivu wa moyo, ustahimilivu, ubinafsi na heshima kwa ustadi wa kikazi huonekana kwa wingi katika methali za Kiingereza. Zaidi ya hayo, methali zilizo na mazingatio ya usawa, haki, kutopendelea na sifa zenye fahari husimuliwa kwa desturi na mara nyingi katika jamii ya Waiingereza, lakini methali hizo hazizingatiwi sana katika masimulizi ya Wakorea. (4) (tafsiri yetu)

Thamani za kimaadili na kijadi zinazohimiza na kujibidiishwa kufuatana na kaida za kijamii hutofautiana kwa sababu ya historia, utamaduni na mazingira tofauti.

Kwa mfano Wakorea wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na falsafa ya Kikonfusiasi ambayo imetapakaa kote Mashariki ya Mbali. Falsafa hiyo ya Kikonfusiasi ilishika mzizi wake katika utamaduni wa kitaifa wa Wakorea na bila shaka ilirutubisha utamaduni wa Wakorea hasa kifalsafa na kimawazo.

Thamani za kimaadili zilizotokana na falsafa hiyo kama vile utii usiobadilika kwa mtawala, unyofu wa mwanamke kwa mume wake, udugu mwema, uthabiti wa uaminifu katika uhusiano wa kirafiki na heshima kubwa yenye adabu njema kwa wazee na wazazi zilipachika na kunyunyiza kwenye nyanja mbalimbali za maisha ya Wakorea. Methali si kivuo (exception), bali methali nyingi zenye kitovu cha falsafa ya Kikonfusiasi huibuka katika matumizi halisi.

Sasa tuangalie mbinu nyingine ya kuziainisha methali ambayo imefanywa na Chung, Chong Hwa (1991);

1. Uhusiano wa Kibinadamu

- a) Ndoa na mume na mke
- b) Mapenzi
- c) Mgeni
- d) Wanawake
- e) Marafiki na majirani
- f) Ukoo

2. Maisha

- a) Kuzeeka
- b) Maisha yasiyodumu daima
- c) Mabadiliko ya maisha yenye kustawi na
Kuporomoka
- d) Kifo

3. Hali ya kuishi

- a) Umaskini
- b) Shida
- c) Njaa
- d) Nguo
- e) Dharura

4. Utajiri

- a) Fedha
- b) Utajiri
- c) Faida

5. Milki

- a) Uyangu
- b) Uya wengine

6. Msimamo katika maisha na silika za watu

- a) Kujiingiza katika mambo ya wengine.
- b) Kujikalifu moyoni
- c) Sura na uhalisi
- d) Uviuu
- e) Unyenyekevu
- f) Tajiriba
- g) Uwekevu
- h) Ujibidiishaji
- i) Jitihada
- j) Ruwaza
- k) Tabia

- l) Silika za watu**
- m) Ujitanadharishaji**
- n) Ugomvi**
- o) Kipeo cha ubora**
- p) Pupa**
- r) Kijicho**
- s) Dhamiri nzuri**
- t) Choyo**
- u) Ustahamiliu**
- v) Ubahili**
- w) Tahadhari**
- x) Ukarimu**
- y) Majivuno**
- z) Ushirikiano**

7. Taadhima na muamana

- a) Taadhima**
- b) Utovu wa shukrani**
- c) Muamana**
- d) Uaminifu**

8. Mwanzo na mwendeleo

- a) Nafasi**
- b) Mwanzo**
- c) Mwendeleo**
- d) Sababu na matokeo**
- e) Udogo na udhaifu**

9. Maneno

- a) Ungamavu
- b) Maneno
- c) Habari
- d) Mapayo
- e) Kutofahamiana
- f) Kisingizio

10. Upungufu

- a) Kutojua
- b) Lisilofaa na lisilostahili
- c) Upungufu
- d) Kutowezezana
- e) Kutokamilika
- f) Ujinga

11. Makosa na majuto

- a) Kusahau
- b) Kupiga mjeledi
- c) Makosa
- d) Matendo maovu
- e) Uhalifu
- f) Majuto

12. Ushirikina na sadfa

- a) Ushirikina

b) Sadfa

c) Bahati

13. Mambo mengine

a) Urahisi na ugumu

b) Utumizi

c) Mamlaka na nguvu

14. Misemo ya kikale

a) Misemo ya kikale (5)

Kama tunavyoona katika mbinu hizo mbili wanatofautiana kwa kiasi kikubwa katika uainishaji na upangaji maudhui mbalimbali chini ya makundi. Kwa hakika wanapoziainisha methali wanaingiza hisia na uamuzi wa mtu binafsi hata ingawa wanatumia nadharia fulani.

Katika kazi yetu hatuunganishi maudhui kadha wa kadha chini ya makundi makubwa, badala ya kujaribu kufanya hivyo tutayaunganisha maudhui yenye dhana zilizo tofauti kabisa. Mfano wa kuweka pamoja methali zenye maudhui yanayofanana na kutangamana kimaana ni kama choyo na ubahili. Hali kadhalika umaskini na utajiri ni mfano wa kuunganisha methali zenye maudhui yanayopingana, lakini yanayohusiana kimaana.

Waidha, hatutaweza kuzipitia methali zote kwa kuwa idadi ya methali ni nyingi hivi kwamba tukijaribu kuziangalia methali hizo nyingi hatutafaulu kuzichambua na kuzihakiki methali hizo kwa undani. Kwa

hivi methali zinazohakikiwa na kuchambuliwa katika kazi yetu ni zile zinazowakilisha na kuibusha sifa mbalimbali za kiutamaduni.

Kwa mfano maudhui yahusuyo swala la maisha na kifo hutiririka kwa namna mbalimbali katika methali, maadamu swala hilo huhusiana na kuambatana na mambo ya kiutamaduni kama vile dini, mila na imani.

Mitazamo ya watu kuhusu maisha na kifo inahitilafiana kwa sababu ya mafundisho na imani za kidini. Kuna mitazamo ya Kibudha, Kikristo, Kiislamu na dini nyinginezo kukabiliana na swala la maisha na kifo.

Ni vigumu sana kupata mbinu kavu ambayo haina hisia za kibinafsi katika taaluma isiyo ya kisayansi. Mbinu ambayo inatunufaisha zaidi inaweza kuchujwa kutoka kwa mbinu mbalimbali zenye maoni na mitazamo jumuishi.

Uainishaji wa methali uliojaribiwa na Albert Scheven(1981) umetumiwa katika kazi yetu. Alitenga makundi ya kimaudhui yapatayo 56 bila kubainisha makundi makubwa na vijikundi vidogo vinauyowekwa chini ya makundi hayo makubwa. Tumeamua kuchagua mbinu yake kwa kuwa siyo rahisi kubainisha dhana ndogo na dhana pana zinazozishika dhana ndogo, bali ni swala la kututatanisha kama inavyoonekana katika mbinu za C.L. Sibusiso Nyembezi (1963) na Chung, Chong Hwa (1991).

Hata hivyo hatutazipuuza mbinu hizo mbili katika kazi yetu, bali zinatupatia mwangaza.

Yafuatayo ni maudhui yatakayoshughulikiwa katika kazi yetu kwa undani kadiri ya uwezo wetu;

- 1) Adabu
- 2) Afya na maradhi
- 3) Bahati njema na bahati mbaya
- 4) Busara na ujinga
- 5) Choyo na ubahili
- 6) Elimu
- 7) Fahari na majivuno
- 8) Haraka
- 9) Hasira
- 10) Kifo na maisha
- 11) Kijicho
- 12) Kisingizio
- 13) Majaaliwa
- 14) Makosa na majuto
- 15) Mapenzi
- 16) Mwanzo na mwisho
- 17) Mwazimo
- 18) Njaa
- 19) Tajiriba
- 20) Uaminifu
- 21) Uhadimu na uhababi

- 22) Ujirani mwema
- 23) Umaskini na utajiri
- 24) Unafiki
- 25) Ushirikiano
- 26) Ushirikina
- 27) Utondoti, siri na unyamavu
- 28) Uvivu
- 29) Uwekevu na akiba
- 30) Uzee na ujana
- 31) Vita na amani
- 32) Wanawake na wanaume
- 33) Wazazi na watoto

3.3. Maana na matumizi ya methali kwa mbinu ya ulinganishi

1. ADABU

50. Aendaye mashambani afuate mila za mashambani.

10z. 51. Akienda katika hekalu ya Kibudha hujifanya mtawa wa kibudha, akirudi mashambani hujifanya kama mlimwengu.

m.z. Methali hii inatufahamisha kwamba lazima tufuate sheria au mila za watu wa mahali ambapo tupo. Ulevile methali ni kinaya kwa mtu ambaye hana msimamo thabiti.

. Wananchi wakila panya, ule panya.

- taaz.* . Ukila pamwe na namiri, igiza zao desturi.
 . Ukenda kwa mwenye chongo nawe vunja jicho
 lako.
 . Ukikaa mji wa wenye chongo nawe vunja lako
 jicho.

52. Mapenzi huota kwenye nchi ya ufito.

m.z. Ncha ya ufito inaashiria kumfundisha mtoto
 au mwanafunzi adabu njema kwa kutumia
 makofi au ufito. Methali hii inahalalisha
 kumwaadhibu mtoto au mwanafunzi kwa njia ya
 kuchapa.

- taaz.* 53. Umchapie mjeledi mwanao umpendaye zaidi,
 umpatie keki ya wali mwanao asiyekupendeza.

* Keki ya wali ni chakula ambacho huandaliwa
 wakati wa sherehe nchini Korea. Hiki hufanana
 na ugali katika umbo lake, lakini hutengenezwa
 kwa unga wa mchele peke yake au kwa
 kuchanganya unga wa mchele na vitu vingine
 kama maharagwe, zabibu na kadhalika.

. Teke la kuku halimwumizi mwanawe.

- taaz.* . Rada ya mwana ni ufito.
 . Ukupigao ndio ukufunzao.
 . Asofundwa na nina, ulimwengu humfunda.
 . Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

2. AFYA NA MARADHI

54. Afya ni bora kuliko mali.

. Lāfiyàr jìkī arzìkī nē. (Methali ya Kihausa)

taf. . Afya ni mali.

. Afya ni bora kuliko mali.

taf. . Bora afya.

55. Aiguapo maradhi ndipo ajuapo huzuni yake.

taf. 56. Huwezi kuthamini uzuri wa afya mpaka uwe mwele.

. Afya ni taji hakuna alijuaye isipokuwa mwenye maradhi.

57. Takabarisha ugonjwa wako.

m.z. Yeyote afichaye ugonjwa wake hatapatiwa dawa wala matibabu. Ni njia nzuri ya kutibu ugonjwa wako ni kufichua na kutangaza ugonjwa huo.

. Mficha ndwele hupati dawa.

taf. . Aendaye kwa mganga hakosi jambo.

58. Dawa nzuri huwa chungu.

m.z. Ingawa maana ya moja kwa moja katika methali hii ni kwamba dawa chungu huwa inaponya maradhi, maana batini ni kwamba mashauri mema yaweza kuwa makali na hayapendezi masikio yako lakini yakunufaisha katika maisha yako.

. Dawa inayowasha inakupenda.

3. BAHATI NJEMA NA BAHATI MBAYA

59. Sakitu inaongezeka juu ya theluji.

ta.z. 60. Kuongeza jalidi juu ya theluji.

61. Nimeanguka na mwingine ameanguka juu yangu.

62. Radi iandamanayo na ngurumo.

63. Anakufa kwa baridi na kwa kuungua.

m.z. Methali hizi hutumiwa kumaanisha msiba au bahati mbaya inayokuja na nyingine iliyo mbaya zaidi.

. Hakuna msiba usio na mwenziwe.

ta.z. . Hapana msiba usiokuwa na mwenzake.

. Hapana msiba usioenda na mwenziwe.

4. BUSARA NA UJINGA

64. Anajenga kasri hewani.

laz. 65. Ni kasri iliyojengwa juu ya mchanga.

66. Kumwanga maji ndani ya kandirinya lililotoboka.

. Mfumbata moshi.

laz. . Acha kujenga nyumba ya karatasi.

. Hujenga ghorofa kuzimuni.

67. Usiuze kuni msituni.

laz. 68. Usitafute sungura baharini.

69. Kuvua samaki mlimani.

70. Aenda mlimani kuuza kuni na baharini kuuza samaki.

71. Usiuze kahawa nchini Brazil.

. Amerudisha tende Manga.

laz. . Amepeleka kilio matangani.

. Chumvi sileteni baharini.

72. Anaokota ufuta baada ya kuyamwaga mafuta ya ufuta.

laz. 73. Baada ya kuteketeza nyumba aokota misumari.

. Kuchinja mbuzi kwa ajili ya kinofu.

laz. . Alivunja jahazi kwa kitumbua.

. Mnunuzi wa mchuzi atalipa mbuzi.

74. Usipepee nyumba inayoteketezwa.

laz. 75. Kumwaga mafuta motoni.

76. Anaingia kwenye nyumba inayoteketezwa akibeba kuni.

. Kuzimisha moto kwa mafuta wilaya.

. CHOYO NA UBAHILI

77. Abaniaye mafua hata hayatoi.

. Joka la mdimu linalinda watundao.

laz. . Joka la mdimu halitundi wala halili, huwasa watundao na walao.

78. Awatafutaye sungura wawili hawezi kumkamata hata mmoja wao.

laz. 79. Aendaye kumwinda ngiri apoteza nguruwe anayefugwa nyumbani.

. Mtaka yote hukosa yote.

laz. . Mwenye kutaka yote hukosa yote.

. Mtaka vyote hukosa vyote

. Bata mtaga mayai usimchinje kwa tamaa ya wingi.

- . Choyo ni shina ya maovu yote.
- . Mchua ngalawa mbili moja humpwelea.
- . Mla kwa miwili hana mwisho mwema.
- . Mla kwa miwili sitakula naye.
- . Mpanda farasi wawili, hujishuka miguu miwili.
- . Mpanda farasi wawili hupasuka msamba.
- . Mshika mbili lazima kimoja kimponyoke.
- . Mshika mbili, moja humponyoka.
- . Mwenza mbili moja humwacha.
- . Tamaa mbili moja itakuponyoka.
- . Mtaka yote kwa pupa hukosa yote.
- . Mtaka yote, mkosa yote.
- . Mpenda yote akosa yote.
- . Mwangaza mbili mbambo mwenga humuengaenga.
- . Mwangaza mbili, moja humponyoka.
- . Mwangaza mbili moja humponya.
- . Njia mbili zaumiza.
- . Njia mbili zilimshinda mzee fisi, alipasuka msamba.
- . Ukioka samaki, huwezi kuondoa manyoya ya kuku.
- . Upepo huchukua vingi na kufikisha kidogo.
- . Usibabue senji wawili.

80. Yawezakana kujaza bahari, lakini haiwezakani
kujaza uchoyo wa binadamu.

laz. 81. Twaweza kujaza bahari, lakini hatuwezi kujaza
moyo wa mwenye choyo.

82. Apandaye farasi ataka kumpata mtumishi

ashikaye hatamu.

m.z. Zamani Wakorea walipanda farasi kwa mawasiliano kutoka mahali fulani hadi pengine. Wananchi wa kawaida hawakuweza kumpata farasi ila maofisa wa kiserikali na matajiri. Mtu anayetembelea hapa na pale kwa miguu akibahatika kumpata farasi hata anashikwa na tamaa ya kumpata mtumishi awezaye kumsadia kushika hatamu. Tamaa ya binadamu haina kikomo.

. Pupa haishi.

tbz. . Pupa halishi.

6. ELIMU

83. Hata *Gongja*(Confucius) humwuliza mtu wa kawaida.

m.z. Confucius (551-479 kabla ya Kuzaliwa kwa Yesu Kristo) alikuwa mwanafalsafa mashuhuri wa China. Alizaliwa katika nchi ya *Lu* iliyokuwa ufalme mmoja nchini China. Falsafa yake iliathiri mambo ya kisiasa na ya kifalsafa katika nchi za Mashariki ya Mbali kama vile China, Korea na Japan. Hata mtaalamu mwenye kiwango cha juu kabisa katika masomo au

utaalamu wake anaweza kupata mambo mengi
asiyoyajua kwa kumwuliza mtu wa kawaida.

laz. 84. Kuuliza ni aibu ya wakati mmoja na kutojua ni
aibu ya maisha mazima.

85. Kuuliza kunakuaibisha wakati mmoja tu, lakini
kutojua kunakufedhehesha kwa muda wote wa
maisha yako.

86. Kuuliza siyo aibu.

. Asiyauliza, hanalo ajifunzalo.

laz. . Jifanye mnyonge upate kujua.

. Kuuliza si ujinga.

. Mtu si mjinga asemaye sikufahamu.

. Muuliza ana ilimu.

. Ukijua huu ule hujui.

87. Kumpatia mwanao *sutra* moja ni bora kuliko
kumrithisha kasha moja linalojaa dhahabu tupu.

* *Sutrani* mojawapo ya misahafu ya Kibudha.

laz. 88. Bora kumpatia mwanao elimu kuliko kumpatia
fedha.

. Elimu ni mali ambayo adui hawezi kuiteka.

laz. . Elimu ndiyo mwanga uongozao kila shani.

. Elimu ni kama taa, gizani itazagaa.

. Mwanavyuoni, shida haoni.

7. FAHARI NA MAJIUONO

89. Mbwa aliyechafuka kwa mavi humdharau mbwa
mwenzake aliyechafuka kwa kumvi za mpunga.

m.z. Tukipimia kiwango cha uchafu mavi
yanazidi kumvi za mpunga. Methali hii
inatufahamisha kwamba mtu mwenye ila au
dosari zaidi kuliko wengine haoni kasoro yake,
bali huwadharau wengine wanaopungua.

taaz. 90. Mwenye dosari kumi amdharau mwenye dosari
moja.

91. Asiye mrembo hulaumu kioo.

92. Alaumu kioo cha kujitazamia bila kujifikiria uso
wake usiopendeza.

93. Mwanamke asiye mrembo huvunja kioo cha
kujitazamia.

94. Mwenye sura mbaya huvunja kioo cha
kujitazamia.

95. Makaa yanayaita mengine mweusi.

. Nyani haoni kundule, huliona la mwenziwe.

taaz. . Nyani haoni kundule, huona la mwenziwe.

. Ajabu ya kondo kucheka kioo.

. Ajabu ya ngamia kucheka nundu ya ng'ombe.

- . Asiyeona aibu zake, haifai aone aibu za wengine.
- . Asoona aibu zake, asione ya mwenziwe.
- . Asoona lake haoni la mwendani wake.
- . Asoona lake na la mwendani wake halioni.
- . Kuni juu ya uchaga zacheka zilizo motoni.
- . Mtu haoni aibu yake, huona ya mwenzake.
- . Lao hawalioni.
- . Nyani haoni ngokoye.

8. HASIRA

96. Lifanyikalo haraka huharibikia haraka.

laz. 97. Wali ulioliwa haraka hukaba koo.

98. Chumba kilichopata moto kwa haraka hupoa kwa haraka.

m.z. Katika nchi nyingi zenye majira ya baridi watu hupenda chumba chenye moto wakati wa baridi. Hivyo basi chumba kikipoa moto kwa haraka si chumba kizuri.

. Haraka, haraka, haina baraka.

laz. . Ka ka ka ka haina mbaraka.

. Kwenda mbio si kufika.

. Mwenda mbio hujikwaa dole.

. Mwenda wa haraka hukwaa dole.

. Linaloinuka haraka ndilo linalokimbia.

. Pole ya kobe humfikisha mbali.

99. Anatayarisha ubeleko kabla hajatunga mimba.

faz. 100. Anajihangaisha na kutayarisha ubeleko kabla hajatunga mimba.

101. Anatayarisha ubeleko kabla hajaolewa.

102. Ashonaye kitambaa chenye kufyonza mkojo na kingesi cha mtoto hata kabla mtoto hajazaliwa.

. No vendas la piel del oso antes de haberlo muerto. (Methali ya Kihispania)

faf. . Usiuze ngozi ya dubu kabla hujamwua.

. Kutinda kanzu mwana hajazawa.

faz. . Wakata kanzu mtoto hajazaliwa.

. Hutafutaje jambia na mtoto hajazawa.

. Usikate ubeleko kabla mtoto hajazaliwa.

. Usikate majani mnyama hajauawa.

. Usikate majani hujaua mnyama.

. Bi. kidumu hulialia, mwenye safari ndoo.

. Bi. kidumu kukulika, mwenye safari begeti.

9. HASIRA

103. Apigaye teke pembe kali ya jiwe huumiza mguu wake.

laz. 104. Hali chakula kwa hasira.

105. Mpigwa teke kwa hasira humiza mguu wake.

106. Chura mwenye hasira hupiga jabalini.

107. Lolote lifanywalo kwa hasira huleta majuto.

. Anger punishes itself. (Methali ya Kiingereza)

laf. . Hasira hujiadhibu.

. Hasira haina macho. (Methali ya Kihindi).

. Mwisho wa hasira ni ukatili. (Methali ya Kiajemi)

. Hasira hasara.

laz. . Ana hasira ya mkizi.

. Hasira ya mkizi furaha ya muuvi.

. Hasira za mkizi tijara ya muuvi.

. Hasira za mkizi furaha kwa muuvi.

. Kukasirika, kughururika.

. Mwenye ghadhabu mbele yake husimama shetani.

. Ukikasirika, utahasarika.

. Ukiwamo ghadhabuni, atakunyata shetani.

10. KIFO NA MAISHA

108. Mbwa aliye hai ni afadhali kuliko waziri aliyekufa.

laz. 109. Afadhali kuwa nguruwe hai kuliko tajiri

alijekufa.

110. Afadhali kuwa mbwa hai kuliko chui wa Bara
Hindi alijekufa.

111. Hata nikifingirika kwenye shamba lililochafuka
kwa mavi ya mbwa napendelea ulimwengu huu kuliko
ahera.

112. Hata nikijibingirisha kwa mavi ya farasi
ulimwengu huu wanipendeza.

. Ni afadhali kuishi kuliko kufa.

laz. . Bora kilema kuliko mfu.

113. Maisha ya binadamu yako mbinguni.

. Kufa kolewa ni Mungu.

laz. . Mambo yote mtenzi Mungu.

. Mambo, mtenzi ni Mungu.

. Mambo, mtenda Rabana.

. Mambo pia kwa Manani.

. Mambo pia kwa Mungu.

114. Nje ya mlango jahanamu iko.

laz. 115. Jahanamu iko kizingitini.

. Kifo ki karibu, ki kishogoni mwako.

116. Kila kiumbe hai lazima atoweke.

. Kifo na kiumbe, kiumbe na kifo.

laz. . Kuna uzima na kifo.

117. Hakuna urefu wala ufupi mbele ya kifo.

laz. 118. Hakuna utajiri wala umaskini mbele ya kifo.

119. Hakuna mashujaa mbele ya kifo.

. Hakuna tajiri shimoni.

120. Mfalme wa Jahanamu akiwa babu yako, huwezi
kujiepusha na kifo.

laz. 121. Hata mfalme wa Jahanamu akiwa baba mzaa wa
mama yako, huwezi kujiepusha na kifo.

122. Buriani ya milele kwa kufa iko mbele ya kila
mlango.

123. Hata tabibu mashuhuri hajiwezi lolote mbele ya
kifo.

. Death is a black camel, which kneels at the gates
of all. (*Abdel-Kader*)

laf. . Kifo ni ngamia mweusi anayepiga magoti katika
milango ya wote.

. Kifo hakina kinga.

laz. . Hakuna kilima bila kaburi.

- . Hakuna mrukaji anayefaulu kuepa kifo.
- . Kifo kikimbizwa funza chawekwa mahali gani?
- . Kiumbe mwisho ni nini?
- . Kufa ni faradhi ya iliyokadirika.
- . Kufa ni faradhi ya kila mtu.
- . Kufa ni njia ya kila kiumbe.
- . Kufa si suna, ni faradhi.
- . Kufa tutakufa wote.
- . Kulala na kufa ni sawa.
- . Mungu hamjui kijana.
- . Mwosha naye huoshwa.
- . Saa haingoji mfalme.
- . Sikio la kufa halisikii dawa.

11. KIJICHO

124. Binamu akinunua shamba la mpunga naumwa tumbo.

m.z. Binamu ni mwana wa ami na kutumia neno 'binamu' kunachukuliwa kuwa msisitizo wa ukaribu wa kinasaba. Kupofuka kwa kijicho hakuji ukaribu wa kinasaba waig damu nzito.

- . Usilie ngoa.

12. KISINGIZIO

125. Seremala asiye hodari hulaumu zana za
useremala.

taz. 126. Asiye hodari wa uchoraji huzichagua brashi.

127. Mlimaji asiye hodari kulima kwa jembe la
kukokotwa na ng'ombe humlaumu ng'ombe.

128. *Shaman* asiye stadi hushutumu *changuyake*.

* *Shamanni* kama mganga wa kienyeji. Yeye
hupunga pepo na kutabiri hatima na maisha ya
watu.

* *Changu* hufanana na ngoma. Hii ni ala ya
muziki inayotumiwa kwa kazi *Shamanna* pia
hutumiwa katika ngoma ya wakulima.

. Mkulima hulaumu jembe lake.

taz. . Alalamikaye kwa wingi hufanya machache.

. Fundi mbaya anateta na ala zake.

. Mchagua jembe si mkulima.

. Mkulima halaumu jembe lake.

. Mshoni hachagui nguo.

. Mchagua mchele si mpishi.

. Mtama ni muwi na wapishi wao.

13. MAJALIWA

129. Mti mzuri hukatwa kwanza.

taf. 130. Mrembo hufariki ulimwengu akiwa mdogo.

131. Majaaliwa ya mrembo ni tufani.

. Beautiful flowers are soon picked. (Methali ya
Kiingereza)

taf. . Maua mazuri huchunwa mapema.

. Chema hakidumu.

taf. . Chema duniani hakina maisha.

. Chema hakikai, hakina maisha.

132. Hakuna dawa mbele ya majaaliwa.

taf. 133. Majaaliwa yako mbinguni.

. Ajali haina kinga.

taf. . Ajali haibishi hodi.

. Ajali haina kinga wala kifara.

. Amekipanda chombo mwamba.

. Cha kuvunja hakina rubuni.

. Chombo cha kuvunja hakina rubani.

. Chombo amekipanaza mwamba.

. Chombo cha kuzama hakina usukani.

. La kuvunja halina rubani.

. La kuvunja halina ubani.

. Liandikwalo ndilo liwalo

. Cha kunja hakina ubani.

- . Liozalo halina ubani.
- . Mja hafuti landishiwelo.
- . Tabibu hazuii ajali.

14. MAKOSA NA MAJUTO

134. Hutengeneza zizi la ng'ombe baada ya ng'ombe huyo kuibiwa.

laz. 135. Baada ya kifo ni dawa.

136. Hutengeneza mlango baada ya kuibiwa.

137. Hufunga mlango baada ya kuibiwa.

- . Baada ya kifo ni tabibu.

laz. . Baada ya nyama haradali.

- . Majuto huja kingume.

- . Majuto ni mjukuu, mwishowe huja kingume.

- . Majuto ni mjukuu, mwishowe huja kinguma.

- . Majuto ni mjukuu, mwishowe huja nyuma.

- . Majuto ni kujukuwa, huja kingumeni.

138. Huhesabu umri wa mwanawe aliyekufa.

laz. 139. Ni maji yaliyomwagika.

140. Ni maji yaliyomwagika na mshale uliofyatulika.

141. Maji yaliyomwagika hayazoleki tena.

142. Ni maji yaliyomwagika na mutungi kibuyu kilichovunjika

- . Maji yaliyomwagika hayazoleki.
- laz.* . Nasibu sitalilia haumiza macho yangu.
- . Iliyopita si ndwele, ganga ijayo.
- . Kama maji yaliyomwagika ndiyo yameshamwagika.
- . Maji yakimwagika hayazoleki.
- . Yaliyopita si ndwele, tuganga yaliyomo na ya jayo.

15. MAPENZI

143. Penye kupendwa pana kupenda.

- . Anipenda nami nampenda: aniketeeo, punguwa simanzi.
- laz.* . Anipendaye, nami nampenda: anikataaye, napunguwa simanzi.
- . Anipendaye, nami nampenda: anikataaye, nami namkataa.
- . Nampenda mtu pindi anipendapo.
- . Mtu akipendwa hupenda.

144. Tatua uadui kwa njia inayofaa.

. Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi.

(Mathayo Mtakatifu 5:44)

. Adui mpende.

laz. . Adui mpende; akikubali ni vita, akikataa huwaje?

. Adui mpende, kumchukia ni kumchukia ndugu yako.

. Adui mpende leo, yawezekana mkawa rafiki kesho.

145. Macho kwa macho, na masikio kwa masikio.

laz. 146. Macho kwa macho, na meno kwa meno.

147. Tawala moto kwa moto.

. Jicho kwa jicho na jino kwa jino. (Mathayo Mtakatifu 5:38)

. Chuki kwa chuki, mwanga kwa mwanga.

laz. . Akutendaye mtende.

. Akutendaye mtende, mche asiyekutenda.

. Akutendaye, mtende: simche akutendaye.

. Dawa ya meno ni meno.

. Dawa ya moto ni moto.

. Sumu ya neno ni neno.

148. Hakuna dawa kwa mtu anayeshikwa na mapenzi.

. Haina tabibu kwa ndwele ya mapenzi.

laz.

. Akipenda chongo huitwa kengeza.

. Akipenda chongo huona kengeza.

. Mapendo yanapovusha.

. Mapenzi hayana macho, wala hayana maarifa.

. Mwenye kupenda ni jura, wala hana maarifa.

149. Mke wako akukupendeza, kunguru anayeketi juu
ya paa ya nyumba ya mke wako pia anakupendeza.

laz.

150. Mke wako akikupendeza wasalimiana hata na
nguzo ya nyumba ya mke wako.

. Ukimtaka Baniani umtake na ubinda wake.

laz.

. Ukipenda damu upende na usaha.

16. MWANZO NA MWISHO

151. Kila chenye mwanzo kiwe na mwisho wake.

. Hakuna chanzo kisicho na mwisho.

laz.

. Kila chenye mwanzo kina mwisho wake.

. Lenye mwanzo lina mwisho.

. Hakuna mwanzo usiokuwa na mwisho.

152. Mwanzo ukiwa mbaya mwisho wake huwa
mbaya.

laz. 153. Mwanzo mwema huwa na mwisho mzuri.

154. Mwaka wa kwanza unapokuwa mzuri mwaka wa mwisho utakuwa mzuri pia.

. Chanzo chema, mwisho mwema.

laz. . Huisha vizuri kianzwacho vizuri.

155. Mwanzo ni nusu ya shughuli.

. Well begun is half done. (Methali ya Kiingereza)

laf. . Lianzwalo vizuri limefanywa nusu yake.

. Mwanzo ni mwanzo hakuna mwanzo mbaya.

laz. . Awali ni awali, hakuna awali mbovu.

. Awali ni awali, awali mbovu hapana.

. Atanguliaye kupiga mara nyingi ni mshindi.

17. MWAZIMO

156. Anapoazima ni *Bodhisattva*, alipapo ni *Yama*

* *Bodhisattva*ni mtakatifu katika dini ya

Kibudha na *Yama*ni mfalme wa jahanamu.

Jahanamu ni jina la moto ambao ni makazi

maalum huko ahera kwa wanadamu waliomwasi

Mungu kwa kutenda maovu duniani; mahali pa

kutisha patakapokuwa na adhabu kali ya moto.

- laz.* 157. **Azimaye kwa tabasamu hulipa kwa hasira.**
 158. **Azimapo hucheka, alipapo hukunja uso wake.**
 159. **Kumkopesha mwandani wako pesa ni
 kumpoteza.**

. **Lending nurses enmity. (Methali ya Kiarabu)**

- laf.* . **Kukopesha huuguza uhasama.**

. **Kukopa arusi, kulipa matanga.**

- laz.* . **Kukopa rahisi, kulipa matanga.**
 . **Mzowea kutwaa, kutoa ni vita.**
 . **Mzowea twaa, kutoa ni vita.**

160. **Mdaiwa wa deni ndiye mwenye hatia.**

- laz.* 161. **Deni hutisha zaidi kuliko chui wa Bara Hindi.**
 162. **Kadiri deni inavyoongezeka ndivyo umaskini
 unavyozidi.**

. **Kukopa kunazaa umaskini.**

- laz.* . **Kanzu ya kuazima usiendelee Ijumaa.**
 . **Nguo ya kuazima haistiri matakao.**
 . **Shoka la mgeni haliwezi kumaliza kazi yako.**

163. Chui wa Bara Hindi akiwa na njaa huweza kula hata towashi.

laz. 164. Chui wa Bara Hindi anayeumia kwa njaa huweza kula hata mhasi.

. Simba akikosa nyama hata majani hujilia.

laz. . Simba akizuiliwa nyama hula majani.

. Mkosa kitoweo humangiria.

. Tusipopata wali tule sima.

165. Njaa na kiu ndicho chakula kitamu .

laz. 166. Mwenye njaa hasikii ladha chungu.

. A buena hambre no hay pan duro. (Methali ya Kihispania)

taf. . Hakuna mkate mgumu kwa mwenye njaa.

. Hunger is the best sauce. (Methali ya Kiingereza)

taf. . Njaa ni mchuzi mzuri kuliko yote.

. Mwenye njaa hana miiko.

167. Hadimu aliyeshiba hukataza kumpikia hababi.

laz. 168. Mkuu aliyeshiba hajui njaa ya mtumishi.

. Ashipaye hamjui mwenye njaa.

laz. . Mtu mwenye shibe hamjui mwenye njaa.

. Kula apataye hajui mwenziwe.

- . Apataye ham jui mwenziwe.
- . Mwenye shibe ham jui mwenye njaa.
- . Aliyeshiba hamkumbuki mwenye njaa.
- . Mwenye shibe hamkumbuki mwenye njaa.

19. TAJIRIBA

169. Waweza kujua shida za wazazi kwa kumlelea mwanao.

laz. 170. Kumlelea mwanao ndiko kuufahamu moyo wa wazazi wako.

. Ng'ombe hajui thamani ya mkia wake mpaka ukatwe.

171. Uinunue dhiki ya wakati wa ujana hata kwa kulipa fedha.

laz. 172. Tajiriba humwezesha hata zuzu awe mwenye busara.

. Uzoefu ndio mama wa maarifa.

173. Huwezi kujua kina cha maji bila kuvuka.

laz. 174. Waweza kukijua kilindi cha bahari kubwa kwa kuvuta tu.

175. Waweza kukijua kina cha maji kwa kuvuka na hali kadhalika uzuri wa mwafulani hujulikana kwa kuingiliana naye.

176. Huwezi kujua urefu wala ufupi kabla hujapima.

177. Huwezi kujua mambo ya ahera kabla hujaaga dunia.

. Kitanda usichokilala, hujui kunguni wake.

taaz.

. Tamu ya muwa aijua muonja.

. Adhabu ya kaburi hujua maiti.

. Adhabu ya kaburi aijuaye ni maiti.

. Adhabu ya kaburi a jua maiti.

. Asiye jua faida ya mwangaza aingie gizani.

. Atangaye sana na jua, hujua.

. Maji usiyoyafika hujui wingi wake.

. Nilale usiku chumbani, nikajua tundu paani.

. Nyumba usiyolala ndani hujui ila yake.

. Nyumba usimolala hujui kama inavuja.

20. UAMINIFU

178. Uaminifu ni hazina ya maisha.

taaz. 179. Mwana wa mwaminifu hafi kwa njaa.

. Muamini hana deni.

taaz.

. Msema kweli hakosi.

- . Habari ya kweli ina ncha moja.
- . Kusema kweli si tua.
- . Kweli ikidhihiri, uwongo hujitenga.
- . Kweli ikisimama, urongo hujitenga.
- . Kweli iliyo chungu si uwongo ulio mtamu.
- . Kweli uchungu, uwongo haramu.
- . Kweli inapofika uwongo hujitenga.
- . Kweli ndiyo fimbo ya kukamata.
- . Kweli ingawa uchungu niambie, usinifiche.
- . Macho ya mbwa hayazui mwanamume kula.
- . Sema kweli, ishi kweli, Peponi utawasili.
- . Ukweli uchungu, lakini wa Mungu.

21. UHADIMU NA UHABABI

180. Chui wa Bara Hindi akiondoka, sungura hujifanya
kama mwalimu.

taz. 181. Kutokuwepo kwa chui wa Bara Hindi kwenye
bonde humfanya sungura ajifanye kama
mwalimu.

. When the boss is not around, we know a lot of
songs. (Methali ya Kiyunani)

taf. . Mkubwa wetu asipokuwa karibu nasi, tunaimba
nyimbo nyingi.

. Paka akiondoka panya hutawala.

taž. . Paka akitoka, panya wataruka.

. Paka wakiondoka, panya watatumilikia.

182. Wadogo humezwa na wakubwa.

. Wakubwa humeza wadogo.

183. Panya mbele ya paka.

taž. 184. Ni kama mwendo wa miguu ya panya mbele ya paka.

. Wewe kisu, mimi nyama.

taž. . Wewe kisu, mimi kipini.

. Wewe jiwe, mimi nazi.

185. Moyo wa wananchi ni wa Mungu.

taž. 186. Sauti ya wananchi ni ya Mungu.

. Mũgambo wa kĩrĩndi no ta wa Ngai. (Methali ya Gĩkũyũ)

taf. . Sauti ya umati ni kama ya Mungu.

. Vóx pópuli vóx Déi. (Methali ya Kilatini)

taf. . Sauti ya watu ni ya Mungu.

. Voz del pueblo, voz del cielo. (Methali ya Kihispania)

taf. . Satu ya wananchi, sauti ya mbingu.

. Penye wengi pana Mungu.

187. Maji ya juu yasipokuwa maangavu, ya chini
hayawezi kuwa maangavu.

taaz. 188. Maji machafu ya juu huyachafua maji ya chini.

. Samaki huanza kuoza kichwani.

taaz. . Samaki inaoza kichwani.

22. UJIRANI MWEMA

189. Heri jirani wa karibu kuliko binamu wa mbali.

taaz. 190. Afadhali jirani aliye karibu kuliko binamu wa
mbali.

m.z. Mtu akabiliwapo na matatizo ya dharura, msaada unaopatikana hata ungawa mdogo sana, hutokana na jirani yake aliye karibu. Methali hii yatilia maanani na umuhimu wa kuwa na jirani mwema akusaidiaye wakati wa dhiki na shida.

. Heri jirani wa karibu kuliko ndugu wa mbali.

taaz. . Jirani wa karibu si ndugu ya mbali.

. Alla, alla, jirani kama ndugu mli kule.

23. UMASKINI NA UTAJIRI

191. Mara uishiwapo na fedha mpenzi wako hutoroka.

taaz. 192. Uishiwapo na fedha, unaachwa hata na rafiki yako.

. Dirishani upendo huruka, umaskini uvukapo kizingiti.

taaz. . Pendo lisilo na kitu, katwa halibainiki.

. Mapenzi ya maskini hayaonekani.

. Mkata hapendi mwana.

193. Maskini huwa na watoto wengi.

taaz. 194. Watoto wengi wako katika nyumba ya maskini.

. Maskini na mwanawe, tajiri na mali yake.

taaz. . Tajiri na maliye, maskini na mwanawe.

195. Yu fukara kabisa hivi kwamba hata apasuke.

taaz. 196. Umaskini unapenya hata mfupani.

196. Hakuna chochote hata kwa kanwa la panya.

197. Yule azamaye majini hana chochote kinachoelea isipokuwa kibeti.

m.z. Kitu chochote kikiwa kizito huzama mara moja ndani ya maji. Kieleacho ndicho kisicho kizito. Kibeti ni mfuko wa fedha unaotengenezwa kwa kutumia ngozi ya wanyama au vitu vingine vilivyo vyepesi.

Kikiwa na ndururu hata moja hakelei. Kwa hivyo kuelea kwa kibeti kunamaanisha kutokuwepo kwa fedha hata ndururu moja.

. Aliyetota, hajui kutota.

taz.

. Hana asili wala fasili.

. Hana asili wala fadhili.

. Maskini hohehahe, hana mbele wala nyuma.

. Asiye na mbele wala nyuma.

. Wanjua ni mkata, sina mbele, sina nyumba.

. Huyu kaja hapa hana mbele wala nyuma.

. Hana mbele wala nyuma.

. Huna mbele wala nyuma.

. Huyu si fidia ya gidamu ya kiatu cha baba yangu.

. Wala si fidia ya makamasi yangu.

. Maskini kama wanamaji wa Bwana Muyaka.

198. Anayeamriwa kumkamata juha humshika fukara.

. Kwa mnyonge hakuna haki.

taz.

. Maskini yoyote asemayo ni makosa.

. Mkata hana kinyongo.

. Mnyonge, msonge.

. Mtu akikosa mali hawi mtu mbele ya watu.

199. Penye fedha tele hapakosi manung'uniko.

taz. 200. Penye fedha nyingi huangaliwa na mwizi.

. Mali mingi adui wengi.

201. Mwenye fedha aweza kununua hasua za bikira.

laz. 202. Hakuna lisilowezezana kwa fedha.

203. Fedha huwezesha kununua makende ya
mwanamwali.

204. Hata mbwa akiwa na fedha huwa waziri.

205. Hata ibilisi hulia mbele ya fedha.

206. Fedha huishinda hata sheria.

207. Lolote haliwezakani bila fedha.

208. Mwenye fedha hufunga na kufungua mlango wa
jahanamu.

209. Akosaye fedha hana mdomo.

. Na divai huyafurahisha maisha;

. Na fedha huleta jawabu la mambo yote. (Mhubiri
10: 19)

. Yote utaweza ukiwa na fedha.

laz. . Fedha ilivunja nguu, milima ikalala.

. Nguu zilivunjika, na milima ikalala.

. Ungwana haufai, bora ni ndarama.

210. Utajiri na umaskini hauwezi kudumu kwa vizazi
vitatu mfululizo.

m.z. Tajiri anaweza kuwa maskini na maskini
anaweza kuwa tajiri kwa kuwa dunia hii ina
mabadiliko yasiyokuwa na kikomo katika kutajirika
na kufukarika.

. Walo wakinuka vumba, leo wako ambarini.

ta.z. . Tajiri huwa fakiri.

. Mwenye mali ndiye mkosa mali.

. Aliyekupa kiti ndiye aliyenipa kumbi.

24. UNAFIKI

211. Anisifuye ndiye adui yangu.

ta.z. 212. Kuna kisu ndani ya tabasamu.

. Akumulikaye mchana usiku akuchoma.

ta.z. . Akumulikaye mchana akuunguza usiku.

. Anayekumulika mchana usiku atakuunguza.

. Akumulikaye mchana usiku hukunyonga.

. Epuka wakusifuo siku zote.

. Akuangaliaye mchana, usiku akuchoma.

. Nyoka ya ndumakuwili, huuma akiuvua.

25. USHIRIKIANO

213. Chombo chenye manahodha wengi huenda
mlimani.

laz. 214. Manahodha wengi merikebu huenda mlimani.

215. Seremala wengi hujengua nyumba.

216. Merikebu ya manahodha wawili huzama.

217. Manahodha wengi huipindua merikebu.

218. Watawa wengi wa Kibudha jikoni huvunja
kandirinya la kupikia wali.

m.z. Wafuasi wa dini ya Kibudha hutembelea hekalu ya Kibudha iliyoko mlimani. Hekalu hizo za Kibudha zimejengwa ndani ya milima mirefu tena mikubwa. Ujenzi wa hekalu ndani ya milima humaanisha ushupavu wa watawa wa Kibudha wanaolazimishwa kujiepusha na kujitengana na mambo ya ulimwengu. Watawa hao hufundishwa kujishughulisha na mambo ya kidini. Kuna kikundi cha watawa wanaofanya kazi ya upishi na usafishaji katika hekalu. Watawa hao huwapikia vyakula wafuasi watembeleo hakalu. Sufuria za kijadi zitumiwazo kupika wali na vyakula mbalimbali hutengenezwa kwa chuma kizito. Sufuria hizo na vifuniko vyao huwa vya rangi nyeusi na vyenye uzito mkubwa. Wanatumia kuni kupasha moto wanapopika vyakula. Sufuria hizo zikipashwa moto mwingi zaidi kuliko kiasi cha wastani chombo hupata nyufa au kuvunjika.

. Nahodha wengi, chombo huenda mrama.

- laz.* . Manahodha wengi chombo huenda mpera.
 . Chombo cha manahodha wengi huzama.
 . Chombo hakiendi ikiwa kila mtu anapiga makasia yake.
 . Manahodha wengi hukiangamiza chombo.
 . Mapaka mengi hayauji panya.
 . Mapaka mengi hayakamati panya.
 . Mipaka mingi hayiindi panya. (Lahaja ya Kiamu)
 . Mapaka mengi hayabwii panya.

219. Utanga viwili vya mikono vipiganapo hutoa sauti.

- laz.* . Mkiinua hata karatasi pamoja itakuwa nyepesi zaidi.

. Kidole kimoja hakivunji chawa.

- laz.* . Bamba la warume, si bamba na maguvu.

. Dau la upweke haliendi joshi.

. Figa moja halitegemezi chungu.

. Jifya moja haliandiki chungu.

. Jifya moja haliinjiki chungu.

. Jifya moja halisimamishi chungu.

. Kijiti kimoja hakisimamishi jengo.

. Mikono miwili ni kuoshana.

. Miwili ndiyo ipakanayo.

. Mkono mmoja haubebi mtoto.

. Mkono mmoja hauchinji ng'ombe.

- . Mkono mmoja haulei mwana.
- . Mkono mmoja hauvunji chawa.
- . Mmoja hashui chombo.
- . Nguzo moja haijengi nyumba.

26. USHIRIKINA

220. Ukikata kucha za vidole usiku mwizi huja.

- . Kukata kucha usiku huleta ufakiri.

221. Kunguru akilia mtu hufa.

laz. 222. Aliapo kunguru ndipo mtu anapofariki ulimwengu.

m.z. Kufuatana na imani ya kijadi ya Wakorea, mlio wa kunguru hubashiriwa na Wakorea kama ndege mbaya wa kuogofya, yaani kifo. Wakorea, hasa wale walioishi katika sehemu za mashambani hutabiri hatima ya binadamu kwa kuangalia urukaji wa kunguru.

- . Bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo.

27. UTONDOTI, SIRI NA UNYAMADU

223. Ndege husikia maneno ya mchana na panya
husikia ya usiku.

taz. 224. Ukuta una masikio.

225. Maneno yasiyo na miguu husafiri //elfu moja.

226. Maneno bila miguu huruka //elfu moja.

m.z. Lini kipimo cha umbali wa masafa ambacho
hutumiwa hasa katika Mashariki ya Mbali. //
moja hukadiriwa kuwa kilometa 3.9273, kwa
hivyo //elfu moja ni kilometa 3927.3.
Wanafasihi wa Kikorea wanapoazimia kusawiri
umbali na masafa, hutumia kipimo hiki. Methali
hii hutumiwa kumtahadharisha mtu asemaye
maneno shaghalabaghala, bila kufikiria kwamba
maneno yake yatatapakaa.

. Wasemapo ndio wasikiapo.

taz. . Ulimwengu hauna siri.

. Hapana siri ya watu wawili.

. Hakuna siri ya watu watatu.

. Macho hayana pazia.

. Siri yako usimwambie mwanamke.

. Siri hailali na njaa.

. Watu siri huibana.

. Masikio hayalali na njaa.

227. Maji yenye kina kirefu huwa yako shwari

m.z. Maji yenye kina kirefu katika methali hii ni mtu ambaye ana ujuzi na mambo mengi. Aghalabu mwenye ujuzi na elimu ya kiwango cha juu hasemi, lakini wajuvi husema mengi ilhali hawayajui.

taz. 228. Chupa inayojaa maji pomoni haitoi sauti.

. Ajuaye mengi hasemi mengi.

taz. . Mtenda mema hasemi, akisema hatendi.

. Debe shinda haliachi kutika.

. Debe tupu haliachi kuvuma.

. Debe tupu haliachi kutika.

229. Penye maneno mengi hapana lenye manufaa.

. Panapo maneno mengi dhambi haikosi.

230. Ulimi ni silaha.

m.z. Methali hii hututahadharisha kwamba maneno mengi yanatuhatarisha.

taz. 231. Shoka limo chini ya ulimi.

. Ulimi unauma kuliko meno.

taz. . Ulimi hauna dawa.

. maneno mengi maradhi.

. Maneno mengi uele (ndwele).

. Maneno mengi ukongo.

- . Maneno mengi huvuta fadhika.
- . Maneno mengi hula akili.

232. Mishale iliyorushwa hupatikana, lakini maneno yakitoka hayarudishwi.

- . Maneno ni kama fumo yakitoka mdomoni hayarudi.

taf. . Shimo la ulimi mkono haufutiki.

28. UUUUU

233. Asiyefanya kazi kwa siku moja wakati wa kifuku (majira ya joto na ungevungevu) atasikia njaa kwa siku kumi katika majira ya baridi.

m.z. Kuna majira manne katika Korea. Majira hayo ni kama vile *spring, summer, autumn* au *fall* na *winter* kwa lugha ya Kiingereza. Wakulima hupanda mbegu majira ya *spring* au *summer* na kuvuna majira ya *autumn*. Asiyepanda majira ya *spring* au *summer* kwa uvivu hawezi kupata mavuno msimu wa kuvuna unapowadia.

- . La ociosidad es madre de todos los vicios.
(Methali ya Kihispania)

taf. . Uvivu ni mama ya maovu yote.

- . Ajizi ni nyumba ya njaa.
- taaz.* . Uvivu ni nyumba ya njaa.
- . Ajizi ni ufunguo wa umaskini.
- . Uvivu na njaa ni ndugu pacha.
- . Kula ni mshahara wa kazi.
- . Uvivu urithisha umaskini.
- . Ukulivu huvuta ufukara.
- . Mvivu hugaguna vifuvu.
- . Mzifu hugaguna zifuvu.

19. UWEKEVU NA AKIBA

- 234. Chembe na chembe huwa mlima mkubwa.
- taaz.* 235. Chembe ya vumbi ikikusanyika huwa mlima mkubwa.
- 236. Chungu angawa mdogo aweza kuijenga ngome.
- . Haba na haba hujaza kibaba.
- taaz.* . Akiba haiozi.
- . Katiti huvaa kingi.
- . Chembe na chembe ni mkate.
- . Kimbuzi na kimbuzi hununua jahazi.
- . Kibuzi na kibuzi hununua jahazi.
- . Tone na tone hujaza ndoo.

30. UZEE NA UJANA

237. Mbwa ambaye amezeeka habweki holera.

laz. 238. Mbwa mzee habweki ovyo ovyo.

239. Mbwa mzee habweki bilashi.

240 Mbwa ambaye amezeeka habweki bila sababu.

m.z. Katika methali hii mbwa mzee

hulinganishwa na mzee ambaye hujua mambo

mengi, yanayopatikana kwa tajiriba yake.

241. Farasi ambaye amezeeka, hapotei njia.

242. Mbweha mzee hanaswi ndani ya mtego.

243. Hupati hasara yoyote kwa kusikiliza maneno ya
mzee.

. Kuishi kwingi ni kuona mengi.

laz. . Chiriku mzee hakamatwi na makapi.

. Mpofuka ukongweni hapotewi na njia.

31. UITA NA AMANI

244. Wapiganapo nyangumi kamba hufa.

laz. . Nyangumi wawili wakipambana, wafao ni
kamba.

246. Nyangumi wawili wapiganapo, ulipukao ni
mgongo wa kamba.

247. Kwenye mapigano ya nyangumi mgongo wa
kamba hulipuka.

. Ndovu wawili wakisongana ziumiazo ni nyika.

taz. . Ndovu mbili zikipambana, liumialo ni gugu.

. Wapiganapo ndovu wawili ziumiazo nyasi.

. Wapiganapo tembo, nyasi huumia.

. Tembo zikipigana huumia nyasi.

. Wapiganapo fahali wawili ziumiazo ni nyasi.

248. Ni muuvi afaidikaye katika mapigano ya korongo
na chaza mwenye makombe mawili.

taz. 249. Ni faida ya muuvi.

m.z. Methali hii inatokana na hadithi ya zamani. Siku moja korongo alikuwa akijaribu kula nyama ilyoko kati ya makombe mawili. Kwa bahati mbaya alipojaribu makombe hayo mawili yaliushikanisha na kuubana mdomo wa korongo. Ilisadifu kwamba walipopigana muuvi mmoja aliyekuwa akipita mahali hapo akabahatika kuwakamata wote wawili bila kutarajia. Methali hii hutumika kwa maana ya kuwa wawili wanapopigana mwingine hubahatika kutokana na mapigano hayo.

. Dita vya panzi ni furaha ya kunguru.

taz. . Dita vya panzi neema ya kunguru.

. Ugomvi wa panzi nafuu ya kunguru.

32. WANAWAKE NA WANAUME

250. Wanawake kumi wakijumuika huweza
kuyeyusha hata chuma.

m.z. Methali hii hutumika kumaanisha kwamba
wanawake hupenda maneno mengi. Penye
wanawake pana mengi.

. Siri moja ambayo wanawake huweza kuificha ni
umri wao. (Methali ya Kiingereza)

. Siri yako usimwambie mwanamke.

251. Nguo ni mabawa.

taf. 252. Hakuna mwenye uso unaochukiza anapovaa nguo
nzuri.

. Kleider machen Leute. (Methali ya Kijerumani)

taf. . Nguo huwapamba watu.

. Clothes make people, priests make brides.
(Methali ya Kiingereza)

taf. . Nguo huwapamba watu, makasisi huwapamba
mabibi arusi.

. Uzuri wa mwanamke ni nguo.

laz.

. Mke ni nguo.

. Mke ni nguo, mgomba kupalilia.

. Uzuri wa mke ni nguo, wa ng'ombe ni kulimiwa.

33. WAZAZI NA WATOTO

253. Mzazi mmoja aweza kuwachukua watoto
kumi, lakini watoto kumi hao hawawezi
kumchukua mzazi yule.

laz. 254. Ingawa kuna mapenzi kwenda chini, hakuna
mapenzi kwenda juu.

255. Mapenzi huenda chini.

. Mwana huu mzee, mzee haui mwana.

laz.

. Kuku havunji yaile.

. Maji huteremkia bondeni, hayapandi kilimani.

256. Utawezaje kumwita baba wa kambo baba wa
kweli?

. Baba wa kambo si baba.

laz.

. Baba wa kambo si baba: kunichukuza mikoba na
ufunguo wa shaba.

. Mama wa kambo si mama.

- . Ukigombana na mama asiye mama yako, ni kuchokoza midomo bure.

257. Damu ni nzito kuliko maji.

- . Damu nzito kuliko maji.
- laz.* . Damu ni damu si karatasi.
- . Isipowasha hunyeza.
- . Azaaye kingago akinyonyesha.
- . Mama hawezi kumkana mtoto, hata akiwa na vilema.
- . Meno ya mbwa hayaumani.
- . Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.
- . Mla nawe hafi nawe, ila kwa mzawa nawe.
- . Mla nae hafi nae, ila kwa mzawa nae.
- . Ndugu mbaya hushinda rafiki mzuri.
- . Ndugu muwi afadhali kuwa naye.
- . Ni nduguyo akuhusuye.
- . Simba hamli mwanawe.
- . Simba na simba hawauani.
- . Wa kuume haukati wa kushoto.

SURA YA TATU

Tanbihi

1. Lee, Ki Moon (1962), Kamusi ya Methali za Kikorea, Seoul:
Il Jo Gak Publishing Co. Uk. 550.
2. Dunham, Dennis (1986), Kumfundisha Samaki Jinsi ya
Kuogelea, Seoul: The Si-sa-yong-o-sa
Publishers Inc. Uk. 50.
3. Ngembezi, C.L. Sibisiso (1963), Zulu Proverbs, Johannesburg:
Witwatersrand University Press. Uk. 48-50.
4. Chung, Chong Hwa, Jarida la Sisa Journal Toleo la tarehe 28
mwezi wa Novemba mnamo mwaka wa 1991,
Seoul.
5. _____ (1991), Kamusi ya Methali za Kikorea-
Kiingereza, Seoul: Tamgudang Publishing Co.
Uk. 9-11.

SURA YA NNE

4.1. Muhtasari wa kiini cha tasnifu

Kwa hakika methali yenyewe ni fasihi ya jumua na falsafa nzito ya maisha. Fasihi andishi kama vile riwaya, insha, mashairi na tamthilia huchukua na kuwakilisha hisia za mwandishi mmoja na fasihi simulizi kama vile kitendawili, methali, majigambo, ngano, hurafa, nyimbo na kadhalika huwakilisha hisia jumuishi za binadamu za jumua. Hii ni sababu mojawapo ya kusema kwamba fasihi simulizi methali ikiwemo ni kioo kidogo cha taifa.

Methali kama fasihi simulizi hudhihirisha wazi wazi huzuni, furaha, hasira, matumaini, kukata tamaa, umaajaliwa na hisia nyinginezo za kibinadamu. (1) Kama tulivyoeleza madhumuni ya tasnifu katika sura ya kwanza utafiti wa methali kama kioo cha jamii utachangia katika juhudi za kufahamu utamaduni wa wanajamii wengine. Kuhusu umuhimu wa methali Lee, Hee Seung (1962) anaeleza kuwa;

Methali ni hazina ya maneno, maua yanayopepetuka katika maneno na nyota inayong'arika katika maneno. Kwa hivyo methali huchukua hekima, hisia na nafsi za taifa. Hivyo basi lazima tuzijue methali ili kulifahamu taifa fulani, na hatutaweza kulijadili na kulifahamu taifa fulani bila kuzielewa methali za taifa hilo. (2)

Tulinuia kutafuta sifa za hisia za kibinadamu kwa njia ya kutalii sura moja ya utamaduni, yaani methali. Mara nyingi mgogoro na mavutano baina ya mataifa mbalimbali husababishwa na ukosefu wa kufahamiana. Badala ya kupanua pengo lililoko la kiutamaduni ambalo huzaa pingamizi katika kufahamiana na kusuhubiana azima yetu ilikuwa kuliziba pengo hilo kwa kuzilinganisha methali zenye kudhihirisha hisia bia za kibinadamu.

Katika kufanya hivyo tulikabiliwa na mambo kadha wa kadha yaliyotutatanisha kwa kiasi kikubwa. Hasa tunapofanya uchunguzi kuhusu methali hatuna budi kuangalia utamaduni na mazingira ambayo yanahusiana na uundaji wa methali. Hata hivyo hatukuweza kuzipitia sura hizo mbalimbali za kiutamaduni kwa sababu ya upungufu wa nafasi na upana wa utamaduni. Ingawaje neno 'utamaduni' linatumiwa kujumuisha mambo mbalimbali kama vile mila, desturi, imani, sanaa, mambo ya kijadi, falsafa na kadhalika upana na udhahania wa neno lenyewe unatutaliza. Kwa sababu hii tukijaribu kuziangalia tanzu hizo nyingi za kiutamaduni tutajikuta tukipotea njia na kuingia msituni.

Aidha ugumu na kutowezekana kuzitafsiri methali nyingi ni tatizo kubwa lililojitokeza. Wanavyosema Agĩkũyũ Rũthiomi rũtigunaga mũthiomerũo (Lugha ya Kigeni haimnufaishi mtu amhitajiye mtafsiri). Maneno ya Kikorea yanayohusu mambo ya kiutamaduni hayapatikani katika lugha ya Kiswahili. Zaidi ya hayo baadhi ya maneno ya Kikorea yanayotokana na mazingira yao hayako katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano mnyama aitwaye 'Tiger' kwa lugha ya Kiingereza haishi katika

Bara la Afrika na neno lenye maana ya mnyama huyo halipo katika lugha ya Kiswahili.

Pamoja na hayo ule utamu wa matumizi ya lugha katika methali ulipotea au ulidhoofika katika kutasfiri. Hizo ni takriri ya sauti na ridhimu. Ijapokuwa hatukuzingatia sana mtindo au fani katika methali, mtindo na fani pia ni muhimu kufahamu maana na ujumbe wa methali.

Vilevile ubinafsi uliingia kwa kiasi kikubwa katika kuziainisha methali kimaudhui. Methali huwa inatumiwa kuwa na maana zaidi ya moja katika miktadha mbalimbali. Tukitoa mifano ya kuthibitisha tatizo hili;

Kutoa ni moyo usambe ni utajiri. (Methali ya Kiswahili). Methali hii yaweza kutumiwa kumsifu mtu kwa utu wake na vile vile kumdhihaki mtu kuhusu ubahili wake. Watu wanaweza kuisema methali hii kuwahimiza watu wafanye wema kwa wenzao.

Hakuna mti wowote usioangushwa kwa makeu kumi. (Methali ya Kikorea) Methali hii inatunasihi kwamba tukifanya juhudi zote kadiri tuwezavyo hakuna lolote lisilowezezana. Pia hutumika kwa maana ya kuwa msichana asiyekupenda hata kidogo akishawishiwa mara nyingi zisizo na idadi atakubaliana nawe.

4.2. Ubia wa hisia za kibinadamu katika methali

Kabla hatujaendelea inatufaa tuziangalie methali zifuatazo;

- . Manahodha wengi huipindua merikebu. (Methali ya Kikorea)
- . Chombo chenye manahodha wengi huenda mlimani. (Methali ya Kikorea)
- . Wapishi wengi huharibu mchuzi. (Methali ya Kijapani)
- . Manahodha wawili hukizamisha chombo. (Methali ya Kiajemi)
- . Wakunga wawili watazalisha mtoto mwenye kichwa kinachopeteka. (Methali ya Kiajemi)
- . Kukiwa na wauguzi saba mtoto hupofuka. (Methali ya Kirusi)
- . Majogoo wengi wakiwika hakutakucha. (Methali ya Kiitalia)
- . Manahodha wengi hukiangamiza chombo. (Methali ya Kiswahili)
- . Manahodha wengi chombo huenda mpera. (Methali ya Kiswahili)
- . Chombo cha manahodha wengi huzama. (Methali ya Kiswahili)

Methali hizi zinafanana kimaana na kutumika kwa maana ya kwamba jambo lolote linaloendeshwa na watu wengi ambo kila mmoja anajifanya kana kwamba yeye ndiye mwenye ujuzi na umahiri wa jambo hilo kuliko wengine litaharibika hatimaye. Ingawa methali hizi zina maneno yanayotofautiana zinatumiwa katika muktadha sawa au

unaolingana. Hata baadhi ya methali hizi zinachukua maneno yaliyo sawa.

Ufanano au usawa huu unatokana na maingiliano ya kihistoria na kiutamaduni au kwa sadfa? Kama tuliyo tangulia kueleza katika sura ya kwanza hakukuwa na mawasiliano ya kibiashara wala kiutamaduni kati ya Korea na Afrika kufikia karne hii. Hata ijapokuwa Wakorea na Waafrika hawakuingiliana kihistoria na kiutamaduni inasadifu kwamba methali za Kikorea na za Kiswahili zilizotajwa hapo juu zinatumia maneno yaliyo karibu sawa ili kuwasilisha dhamira zao.

4.3. Mapendekezo

Ingawa hii ni kazi ya uasisi na kazi ya uasisi, kwa kawaida, huwa si kamilifu, tunaamini kwamba kazi yetu itakuwa mchango usioweza kupuuzwa katika kuziba pengo la kutofahamiana na kuleta mshikamano wa kiutamaduni.

Kufahamiana kwa utamaduni kunaasisi kwa karne mpya ya amani ya dunia na usawa wa binadamu wote. Wakoloni na mabeberu walibainisha utamaduni wao na utamaduni wa Ulimwengu wa Tatu. Walisadiki kwamba utamaduni wao ndio ustaarabu na kwamba utamaduni wa Ulimwengu wa Tatu ni ushenzi ambao utupwe mbali. Fasihi simulizi methali zikiwemo zimeporojwa na wakoloni na hata wakazidharau.

Korea ilikuwa chini ya ukoloni wa Japan kuanzia mnamo mwaka wa 1910 mpaka mwaka wa 1945. Mbali na uvamizi wa kijeshi, kisiasa na kiuchumi wa wakoloni wa Japan walitumia sera ya kutokomeza utamaduni wa kitaifa wa Wakorea. Walipiga marufuku matumizi ya lugha ya Kikorea na ufundishaji wa historia ya Korea shuleni. Wakoloni hao waliwalazimisha Wakorea wabadilisha majina yao yawe ya Kijapani. Magazeti na majarida yaliyokuwa yakitolewa kwa lugha ya Kikorea yalipigwa marufuku. Wale wanachama wa Chama cha Uchunguzi wa Lugha ya Kikorea walipelekwa gerezani.

Wakoloni wa Japan walijaribu kutokomeza utafifa wa Kikorea na utamaduni wao. Lakini wazalendo wa Korea hawakupiga magoti, bali walitumia kila njia kuisambaza lugha ya Kikorea na kuhifadhi utamaduni wao. Ingawa wakoloni wa Japan walifaulu kuiweka nchi ya Korea chini ya utawala wao walishindwa kutokomeza utamaduni wa Wakorea.

Kenya na Tanzania pia zilikuwa zikitawaliwa na wakoloni wa Uingereza na Ujerumani. Mambo mengi ya kijadi yalididimia na kupuuzwa na wakoloni kama ushenzi. Wakoloni walifundisha watawaliwa waamini kwamba utamaduni wa kitaifa ni duni na utamaduni wa kikoloni ni bora zaidi. Tukiangalia hali ya lugha ya Kiswahili jambo hili ladhahirika wazi wazi. Tunashuhudia wananchi wengi wakiipuuza lugha ya Kiswahili. Hisia za unyonge kuhusu utamaduni na lugha zinasababishwa na nini?

Watu wengi wanaiga mambo ya kigeni kama kasuku bila kupekua dhamira wala kuona kasumba yake. Wanajikanusha na kujidunisha kwa kuhafifisha utamaduni wao na kuyaiga mambo ya kigeni. Wanapotambua utukufu wa utamaduni wao na mambo ya kijadi ndipo wanapoweza kujitukuza kama mjenzi wa hatima yake katika ulimwengu huu.

Kwa hivyo, ni muhimu sana kutambua umuhimu wa utamaduni wa kitaifa. Methali inachukua nafasi muhimu sana katika uchunguzi wa utamaduni wa kitaifa. Tunaweza kujua hekima za mababu zetu katika methali. Katika utafiti wetu tuligundua baadhi ya vizuizi vinavyotufinya. Utatuzi wa vizuizi utakuwa mapendekezo yetu.

Mwamko kuhusu utamaduni wetu unahitajika kuhuisha utamaduni wa kijadi ya kitaifa. Ujenzi wa utamaduni mpya hautawezekana kamwe bila kuutathmini utamaduni wa kijadi. Ili kutimiza lengo hili timilifu, inatubidi kuondoa kasumba ya ukoloni mambo leo ambao utatuhimiza tuhisi hisia za unyonge kuhusu utamaduni wetu na kutudunisha. Tukijivunia utamaduni wetu wa kitaifa pasi na utambuaji na utathmini wa thamani za mambo ya kijadi tuliyorithishwa na mababu zetu, fahari haitaweza kuchukua nafasi yoyote. Lazima tutafsiri utamaduni wa kijadi upya kulingana na muktadha wa jamii ya kisasa.

Tunawajibika pia kuendeleza mawasiliano ya kiutamaduni kati ya Korea na nchi za Afrika ya Mashariki. Tulipofanya uchunguzi wa methali za Kikorea na za Kiswahili tulipatwa na matatizo mengi

yaliyotukwamisha njiani. Matatizo hayo ni kama vile kutokuwepo kwa makala, vitabu, na majarida mbalimbali yanayoshughulikia utamaduni wa Wakorea kwa lugha ya Kiswahili. Historia na utamaduni wa Wakorea zitafsiriwe kwa lugha ya Kiswahili hali kadhalika historia na utamaduni wa Waswahili zitafsiriwe kwa lugha ya Kikorea. Kwa kufanya hivyo tutafanikiwa kuihakiki mada maalum na kufahamu utamaduni wa Wakorea na Waswahili.

Na wataalamu wengi zaidi wafanye uchunguzi na uhakiki wa fasihi simulizi kwa upana na undani zaidi. Kazi nyingi zilizofanywa mpaka siku hizi zilikuwa kuzikusanya na kuzieleza maana za kazi za fasihi simulizi tu. Tutaweza kuinua kiwango cha uchunguzi wa fasihi simulizi kwa mbinu ya uhakiki na uchambuzi. Ndipo tutaweza kugundua ubia wa hisia za kibinadamu.

Hapa tunataja baadhi ya mambo ambayo yamekuwa vizuizi katika uchunguzi wa fasihi simulizi methali zikiwemo. Kwanza sera ya elimu yapaswa kubadilishwa. Elimu ya nyanja mbalimbali za fasihi simulizi haijatolewa shuleni kama somo muhimu. Sera ya elimu ihimize mafundisho ya elimu ya kitaifa ili wanafunzi waweze kuutambua utukufu wa utamaduni wa kitaifa. Dilevile hatua imara ichukuliwe kuondoa fikira za ukoloni na kasumba ya ukoloni mambo leo.

Pili wasomi wenye hisia za kikoloni na viongozi waliokengeushwa kiakili wanawajibika kubadilisha msimamo na mtazamo wao. Mabadiliko ya msimamo na mtazamo hayawezekani bila kujitambua na kutathmini utamaduni wa kitaifa.

Tatu uvivu wa wachunguzi wa fasihi simulizi umekuwa sababu moja ya kuukwamisha uchunguzi wa fasihi simulizi. Moyo wa kujitolea utaweza kuukwamua uchunguzi wa nyanja mbalimbali za fasihi simulizi. Itawalazimu wataalamu kuoanisha nia yao na vitendo halisi.

Nne msaada wa kifedha wahitajika kuwawezesha wachunguzi kufanya uchunguzi mpana na kuzichapisha kazi zao ziwe vitabu.

Mwisho tunatumaini mapendekezo yetu hayatukuwa weweseko bali yatatekelezwa yawe mchango usio mdogo wala hafifu katika jitihada za kufahamiana. Kazi yoyote haiwezi kuwa kamilifu na ina udhaifu wake, hivyo basi pengo la udhaifu na dosari katika kazi yetu lazima lijazwe na wasomi wenzetu.

SURA YA NNE

Tanbihi

1. Tukiziangalia baadhi ya methali zinazoonyesha hisia hizo;

a) Dhihaka kwa wanaotawala na mataifa makubwa

. Ndovu wawili wakisongana ziumiazo ni nyika. (Methali ya Kiswahili)

. Wapiganapo nyangumi wawili aumiaye ni kamba.
(Methali ya Kikorea)

b) Uhakika kuhusu ushindi wa mambo ya haki

. Hakuna atajirikaye kwa mapato yasiyo ya haki. (Methali ya Kihispania)

c) Matumaini na matarajio.

. Penye giza patageuka pawe penye mwangaza. (Methali ya Kikorea)

. Siku moja upate kilango cha jaha. (Methali ya Kiswahili)

d) Huzuni ya mnyonge

. Kwa mnyonge hakuna haki. (Methali ya Kiswahili)

e) Umaajaliwa.

. Umaskini ni jaala. (Methali ya Kikorea)

2. Lee, Hee Seung (1962), Zinduo katika **Kamusi ya Methali za Kikorea**, Seoul: Il Jo Gak Publishing Co.

MAREJEO

Abdulaziz, Mohamed H. (1979), Muyaka 19th Century Swahili

Popular Poetry, Nairobi: Kenya Literature

Bureau.

Abudu, Maryam/Barwa, Abdalla (1981), Kitabu cha Pili Methali

za Kiswahili Maana na Matumizi, Nairobi:

Shungwaya Publishers Ltd.

_____ (1981), Kitabu cha Tatu Methali za

Kiswahili Maana na Matumizi, Nairobi:

Shungwaya Publishes Ltd.

Ameir Issa Haji/Ali Mbarouk Mzee/Buhma M. Naaman/Asia Abdalla

Mbarouk (1983), Fasihi Simulizi Zanzibar Kitabu cha

Kwanza, Dar es Salaam: Tanzania Publishing

House.

Amos, Ben Dan (1976), Folklore Genres, Austin: University of

Texas Press.

Bakhressa, Salim K. (1992), Kamusi ya Maana na Matumizi,

Nairobi: Oxford University Press.

Buton, Richard F. (1969), Wit and Wisdoms from West Africa;

A Book of Proverbial Philosophy, Idioms,

Enigmas, and Laconisms, New York: Biblo and Tannen.

Choe, Geun Hak (1986), **Kamusi ya Methali za Kikorea**, Seoul: Munhak Publishing Co.

Choe, Sang Su (1983), **Annual Customs of Korea**, Seoul: Seomundang Publishing Co.

Chung, Chong Hwa (1991), **Kamusi ya Methali za Kikorea-Kiingereza**, Seoul: Tamgudang Publishing Co.

Chung, Joo Young (1987), **Ufafanuzi wa Methali za Kikorea-Kiingereza**, Seoul: Hakil Publishing Co.

Chung, Kyung Cho /Phyllis Haffner/Fredric Kaplan (1988), **The Korea**, Teaneck: Eurasia Press.

Chun, Shin Yong (ed.) (1982), **Korean Cultural Series 4, Folk Culture in Korea**, Seoul: The Si-sa-yong-o-sa Publishers, Inc.

_____ (ed.) (1982), **Korean Cultural Series 9, Customs and Manners in Korea**, Seoul: The Si-sa-yong-o-sa Publishers, Inc.

- Chuo Kikuu cha Uchumi na Biashara (Idara ya Kikorea) (1986),
Kamusi ya Methali za Kikorea, Peking.
- Clark, Virginia P./Eschholz, Paul A./Rosa, Alfred F (eds.) (1981),
Language Introductory Readings Third
 Edition, New York: St Martins Press Inc.
- Covell, John Carter (1981), **Korea's Cultural Roots**, Salt Lake
 City: Moth House Publications.
- Dae Kyung Publishing Company (ed.) (1987), **Kamusi ya
 Methali**, Sihung.
- Dunham, Dennis (1986), **Kumfundisha Samaki Jinsi ya
 Kuogelea**, Seoul: The Si-sa-yong-o-sa
 Publishers, Inc.
- Farsi, S.S. (1958), **Swahili Sayings from Zanzibar**, Nairobi:
 Kenya Literature Bureau.
- Finnegan, Ruth (1970), **Oral Literature in Africa**, Nairobi:
 Oxford University Press.
- Grant, Bruce K. (1982), **Korean Proverbs**, Seoul: Wu Ah Dang
 Publishing Company.

- Hakwonsa Ltd. (ed.) (1960), **Korea its Land, People and Culture of all Ages**, Seoul.
- Harries, Lyndon (1965), **Swahili Prose Texts**, London: Oxford University Press.
- Ha, Tae Hung (1958), **Korean Cultural Series-Dol. VII, Maxims and Proverbs of Old Korea**, Seoul: Yonsei University Press.
- Ilyon (1972), **Samkuk Yusa (The History of the Three Kingdoms)**, Tafsiri ya Ha, T.B./Mintz, G.K., Seoul: Yonsei University Press.
- Jaspers, Karl (1962), **Socrates, Buddha, Confucius, Jesus**, New York: Harcourt, Brace and World, Inc.
- Kamera, W.D. (1983), **Fasihi Simulizi na Uandishi katika Shule za Msingi**, Makala Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya *Waandishi wa Kiswahili III Fasihi*, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Karama, S./Saidi, M. (1983), **Maelezo ya Methali za Kiswahili**, Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Khamis, Hamad Asha (1981), **Tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi**, Makala katika Misingi ya Nadharia ya Fasihi, Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.

Khamis, S.A.M. (1983), **Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania**, Makala katika Mulika Na. 15, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kim, Dae Jung (1984), **Nyaraka za Kim Dae Jung kutoka Gerezani-Nikiikumbatia Huzuni ya Kitaifa**, Seoul: Chǒngsa Publishing Co.

King'ei, Geoffrey Kitula (1982), **Uhakiki wa Nthimo (Methali) za Kikamba, kwa Kufuatisha Misingi ya Methali za Kiswahili** (Tasnifu ya shahada ya M.A., haijachapishwa), Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Knappert, Jan (1979), **Myths and Legends of the Swahili**, Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.

Korean Overseas Information Service (ed.) (1991), **Facts about Korea**, Seoul.

Leach, Maria/Fried, Jerome (eds.) (1950), **Standard Dictionary of Folklore, Mythology, and Legend**, New York: Funk and Wagnalls Co.

Lee, Elizabeth K. (1989), **The Koreans**, Seoul: Korean Overseas Information Service.

Lee, Jung Young (1982), **Sokdam Capsules of Korean Wisdom**, Seoul: Seoul Computer Press.

Lee, Ki Moon (1962), **Kamusi ya Methali za Kikorea**, Seoul: Il Jo Gak Publishing Co.

Lee, Kyu Tae (1987), **Taaluma ya Korea ya Machozi**, Seoul: Kirinwon Publishing Co.

Matteru, M.L. Balisidya (1981), **Uchunguzi katika Fasihi Simulizi: Dizingiti na Mkabala**, Makala Katika Makala za Semina ya Fasihi Simulizi, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

(1983), **Fasihi Simulizi na Uandishi wa Kiswahili**, Makala Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III Fasihi, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mbaabu, Ireri (1985), Utamaduni wa Waswahili, Nairobi:

Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd.

Minjung Publications Ltd. (ed.) (1989), Kamusi ya Kikorea

Sanifu, Seoul.

Mlacha, S.A.K. (1981), Methali kama Chombo Muhimu katika

Jamii, Makala Katika Makala za Semina ya Fasihi Simulizi,

Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu
cha Dar es Salaam.

Mponda, M.S.S. (1975), Fasihi Simulizi, Makala katika Mulika

Na. 7, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa

Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Msuya, Peter A. (1977), Fasihi ya Methali, Makala katika

Mulika Na. 9, Dar es Salaam: Chuo cha Uchunguzi

wa Lugha ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es
Salaam.

Mtesigwa, P.C.K. (1989), Methali ni Nini?, Makala katika

Kiswahili Juzuu 56, Dar es Salaam: Taasisi ya

Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es
Salaam.

- Mulokozi, M.M./Kahigi, K.K. (1979), **Kunga za Ushairi na Diwani Yetu**, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M.M. (1983), **Utafiti wa Fasihi Simulizi**, Makala Katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III Fasihi, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Ndalu, Ahmed/King'ei, Kitula G. (1989), **Kamusi ya Methali za Kiswahili**, Nairobi: Heinemann Kenya Ltd.
- Njũrũri, Ngũmbu (1983), **Ġĩkũyũ Proverbs**, Nairobi: Oxford University Press.
- Ngembezi, C.L. Sibusiso (1963), **Zulu Proverbs**, Johannesburg: Witwatersrand University Press.
- Oliver, Roland/Mathew Gervase (1963), **History of East Africa** Vol 1, London: Oxford University Press.
- Omari, C.K./Kezilahabi, E./Kamera, W.D. (1975), **Misemo na Methali toka Tanzania I**, Arusha: East Africa Publications Ltd.

Pace International Research, Inc. (ed.) (1983), Main Currents of Korean Thought, Arch Cape.

Pares, Susan (1985), Korean and Western Culture in Contrast Cross-currents, Seoul: Seoul International Publishing House.

Parker, Carolyn Ann (1974), Aspects of a Theory of Proverbs: Contexts and Messages of Proverbs in Swahili (Ph.D. dissertation), Washington: University of Washington.

(1981), Tamathali za Usemi katika Methali za Kiswahili: Takriri, Makala Katika Makala za Semina ya Fasihi Simulizi, Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Saidi, M. (1976), Fani Mbalimbali za Kiswahili, Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Scheven, Albert (1981), Swahili Proverbs, Washington: University Press of America, Inc.

Sehwa Publishing Co. (1985), English-Korean Proverb Dictionary, Seoul.

Seligson, Fred Jeremy (1986), Some Thoughts on *Taogu* in
Journal of Hankuk University of Foreign Studies
Vol. 19, Seoul: Hankuk University of Foreign
Studies Press.

(1989), Oriental Birth Dreams, New Jersey:
Hollym International Corp.

Senkoro, F.E.M.K. (1982), Fasihi, Dar es Salaam: Press and
Publicity Centre.

Song, Jae Sŏn (1983), Kamusi Kuu ya Methali za Kikorea,
Seoul: Seomundang Publications Ltd.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (wah.) (1983), Kamusi ya
Kiswahili Sanifu, Dar es Salaam.

wa Mũtiso, Kineene (1987), Utamaduni wa Wakorea, Seoul:
Shirika la Uchapishaji la Chuo Kikuu cha Masomo
ya Kigeni cha Hankuk.

/Yang, Chul Joon (1988), A Dictionary of
Swahili-English-Korean Proverbs, Seoul:
Myaung Ji Publishing Co.

wa Thiong'o, Ngugi (1981), Writers in Politics, Nairobi:
Heinemann Educational Books Ltd.